# Nipashe

Jumatano Desemba 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581894

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


UKURASA WA 3

**Makamu** Rais Z'bar: Utitiri wa kodi na wasimamizi wengi vinawatesa walipaji

UKURASA WA 4

RIPOTI MAALUMU -3

**Kilichokutwa** shule jirani na makaburi kinavyokinzana na maelekezo serikalini

UKURASA WA 3

**Toto** Afya Kadi rasmi na vifurushi vyake kibao



UKURASA WA 22

**MAGUIRE: NITABAKIA MANCHESTER UNITED**

## ALIYENG'ATWA NA NYOKA...

# Afia kituo cha afya kisa hana 150,000/-

• **Mume** alidhamini pikipiki akatafute fedha, akagomewa... *Uk. 2*



## Lissu achukua fomu akiwajibu wanaomkosoa

UKURASA 2

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akimkabidhi Tundu Lissu (Makamu Mwenyekiti Bara), fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa chama hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

## Bwana harusi aliyetoweka akutwa kwa mganga Pemba

UK. 18

UK. 3



**MSAJILI WA VYAMA TENDWA AFARIKI DUNIA**

**MICHEZO** MRITHI WA DIARRA ATAFUTWA YANGA UK.24

**MAONI,** UK.6



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akibadilishana hati ya mkataba na Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mapato Oman, Nasser Al-Jashmi, unaohusu makubaliano ya kuondoa utozaji kodi ya mapato mara mbili na kuzuia ukwepaji kodi. Hafla iliyofanyika jana makao makuu ya Mamlaka ya Kodi, Mjini Muscat, Oman. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

ALIYENG'ATWA NA NYOKA...

# Afia kituo cha afya kisa hana 150,000/-

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

KATIKA hali ya kusikitisha, mkazi wa Magugu, Wilaya ya Babati, Juliana Obedy (44), amepoteza maisha baada ya wataalamu katika Kituo cha Afya Magugu, kudaiwa kumcheleweshea huduma kituoni hapo kutokana na kugongwa na nyoka.

Imedaiwa kuwa, sababu za kucheleweshwa kwa huduma hiyo ni wataalamu kutaka kulipwa Sh. 150,000 ikiwa ni gharama za matibabu.

Akisimulia mkasa huo jana, mume wa Juliana, Obedy Laizer, alisema Desemba 16, mwaka huu, akiwa anavunja jengo la Kanisa la Katoliki Magugu, mke wake alipita akiwa anachuma mboga za majani na kung'atwa na nyoka ambaye hakujua ni wa aina gani.

Laizer alisema baada ya muda mfupi mke wake kuondoka, alikuja mtoto wake na kumwambia anaitwa na mama yake ambaye alidai kung'atwa na nyoka, ndipo alipokimbia kumpeleka Kituo cha Afya Magugu.

Alipomfikisha kituoni hapo kulikuwa na foleni na kushauriana na mke wake waingie ndani na kujisajili, lakini wauguzi waliwaambia kuwa daktari alikuwa chumba cha wazazi na kuomba apigiwe simu ili kuja kumsaidia.

"Daktari alipigiwa simu mara ya kwanza hakupokea, akapigiwa simu mara ya pili ndipo alipopokea akasema anakuja na alitoa huduma na mgonjwa kuandikiwa dawa," alisema Laizer.

Hata hivyo, alisema alipoenda duka la dawa aliambiwa anatakiwa kulipia Sh. 150,000 ambapo Laizer aliomba mgonjwa ahudumiwe na fedha itafuata, lakini wauguzi wawili na daktari mmoja waliokuwapo hawakukubali na kuamua kumpigia Mganga Mfawidhi simu na kujibiwa kuwa anatakiwa alipie Sh. 150,000 na kukata simu.

Laizer alisema baada ya kuvutana na wataalamu hao alitoka na kwenda kutafuta fedha aliporudi alitoa Sh. 130,000 na badala ya kuanza kutoa huduma, wataalamu hao walianza kupigiana simu ndipo mmoja alisikika akisema mgonjwa ahudumiwe.

Aidha, alisema baada ya kulipia fedha hiyo muuguzi anayehusika na dawa alimpeleka duka la dawa na kumpatia na walirudi kwa mgonjwa ambako alifukuzwa wodini, lakini aligoma akitaka kushuhudia mke wake akihudumiwa.

Alisema mgonjwa aliulizwa anajisikiaje naye akajibu kuwa anajisikia vibaya huku akisema "Bwana Yesu nisaidie" ghafla aliacha kuongea na ndugu na majirani waliokuwapo walianza kumwombea kwa kushirikiana naye bila mafanikio.

Alisema baada ya mke wake kukata kauli wauguzi waliendelea kumchua na kumwekea oksijen, lakini alipoona haisaidii aliwaambia waitoe.

"Baada ya kuona hivyo niliwaambia mke wangu ndio anaondoka hivyo, tulienda duka la dawa wakanipa dawa ya Sh. 6000 ya kumpunguzia maumivu na sikupewa risiti, wala ile ya 150,000 sikupewa," alisema.

Akiongea kwa uchungu alisema licha ya kuwaomba aweke rehani pikipiki yake na kuwapa funguo wauguzi ili wamhudumie mke wake waligoma na kudai akikimbia wao ndio wanawajibika.

Mtoto wa marehemu, Abednego Obedy, alisema mama yake alimwonesha mkono ukiwa umevimba na kumwambia ameng'atwa na nyoka na kumshauri kwenda kituo cha afya.

Aidha, Enoti Philipo ambaye alikuwa akimwita marehemu shangazi, alisema alitoka nyumbani kwake kuchuma mboga za majani na baadaye aliona mume wake anamkimbiza hospitali.

Mkazi wa kijiji hicho, Yona Laizer, alisema kitendo kilichofanywa na wataalamu hao ni uzembe na unyama ambao kama wakiendelea watasababisha vifo vingi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Magugu, Lohay Amos, alilaani tukio hilo na kuwataka wauguzi na madaktari kutii viapo vyao.

Akizungumzia tukio hilo kwa njia ya simu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Magugu, Dk. Kusta Ndunguru, alikiri kupigiwa simu na Laizer huku akisema alijua anathibitisha malipo aliyoambiwa.

Dk. Ndunguru alisema alimwambia aongee na wataalamu waliopo hospitali ili wamsaidie kwa kuwa yeye yuko nje ya kituo na hakumrudia.

Alisema mtu aking'atwa na nyoka mwenye sumu kali haitakiwi kuzidi nusu saa kwasababu ikizidi anapoteza maisha ndio maana alimwambia awaeleze wataalamu ili wamsaidie asipoteze muda.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email:customerrelations@guardian*

# Lissu achukua fomu, awajibu wanaomkosoa

**Na Romana Mallya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu amechukua fomu kugombea nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho huku akiwajibu watu wanaokosoa uamuzi wake na kusema jambo hilo si la ajabu na kuwahoji walitaka achukue nani.

Akizungumza jana asubuhi nyumbani kwake Tegeta, Dar es Salaam, kabla ya kwenda kuchukua fomu, Lissu alisema siyo ajabu yeye kugombea nafasi hiyo na wala kupambana na mwenyekiti wake (Mbowe).

Katika mahojiano hayo na kipindi cha Power Breakfast cha Clouds FM, Lissu alisema kitu ambacho watu wanakiona cha ajabu ni yeye kuwa Makamu Mwenyekiti na kutangaza kuchukua fomu ya uenyekiti CHADEMA.

"Sasa mlitaka achukue nani kama siyo Makamu Mwenyekiti? Nani ndiye aliyeandikiwa kuchukua na nani asichukue? Kinachoonekana cha ajabu ni hicho tu," alisema.

"Kinachoonekana cha ajabu ni hicho tu na Mwenyekiti mwenyewe hajasema kama anagombea. Kelele yote ni kwa sababu mimi nimesema wakati mwenyekiti hajasema. Msingi wa kelele hizo kisheria na katiba ya chama hakuna na hata nikigombea, nisipochaguliwa nitakuwa sijawahi kuwa mwenyekiti wa chama, nikichaguliwa nitakuwa mwenyekiti wa nne CHADEMA," aliongeza.

Lissu alisema hana ugomvi wala vita na Mbowe au viongozi wengine wakuu CHADEMA ndiyo maana baada ya kutangaza nia yake, waliketi pamoja katika kikao cha kamati kuu ya chama hicho.

Kuhusu madai ya rafu zilizowahi kutokea wakati wa uchaguzi wa kanda wa chama hicho endapo kama hafikirii zitatokea katika uchaguzi wa Januari, Lissu alisema kama zilitokea ngazi ya chini zinaweza kutokea ngazi za juu.

"Watu wanasema kwa nini unasema haya hadharani. Yasiposemwa hadharani yasemewe wapi? Tuna mwongozo dhidi ya rushwa ndani ya chama ambao umeingiza makatazo yote ya rushwa ya uchaguzi yaliyoko katika sheria za nchi," alisema.

**KUHAMA CHADEMA**

Kuhusu endapo ikatokea katika uchaguzi huo akashindwa kwa hila atafanya nini, Lissu alisema: "Kwanza niweke wazi maana yake kuna vimaneno maneno huyu anatengeneza namna ya kuhama. Kwanza, hahami mtu."

Lissu alisema yeye ni mwanamageuzi na kudai kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM), hakijawahi kuwa chama cha mageuzi na hakitakaa kiwe. Alisema ana miaka 20 ndani ya CHADEMA tangu alipojiunga, kwamba kuna damu, jasho na fedha yake kidogo.

Lissu alisisitiza kwamba kama kuna hila, udanganyifu au kuingiliwa hayo ni mambo ambayo hajawahi kuyanyamazia na kuahidi hatofanya hivyo.

Alipoulizwa kama anadhani mfumo utafurahia awe mwenyekiti, Lissu alisema: "Sina shaka hata kidogo kwamba mfumo hauwezi. Kama mfumo una maana hawa watawala ambao wamekuwapo madarakani ambao wamekuwapo zama zote hizi, hawawezi kufurahi mimi kuwa madarakani. Kwa taarifa yako wameshaanza".

Katika mahojiano hayo, Lissu pia alielezea kuhusu andiko lake aliloliweka katika akaunti ya X juzi inayozungumzia watu wasiojulikana wanaotaka kumdhuru ili wamsingizie mwenyekiti wake, Mbowe.

"Juzi kuna mtu mmoja alinitafuta naomba nihifadhi jina lake, tangu nilipotangaza habari hii (kugombea uenyekiti). Alipiga simu zaidi ya mara 10, ninafahamiana naye ni mtu mkubwa sana na wa heshima sana.

"Si mtu wa kuzusha maneno, si kiongozi serikali, lakini ni mtu mkubwa sana katika nchi hii. Jana (juzi) nikaangalia simu yangu nikakuta miss call nyingi sana za huyu baba.

"Nikamtafuta mawasiliano hayakuwa mazuri alikuwa safarini, lakini jioni tukapata mawasiliano mazuri akanipigia akaniambia 'nimekutafuta sana jana na nimekutafuta kukuambia tafadhali ongeza ulinzi', alisema na kusisitiza waliwasiliana kwa whatsApp.

Lissu alisema baada ya taarifa hiyo, alipomuuliza mtu huyo kama anamruhusu kutangaza suala hilo alimruhusu, ndipo alipoamua ku-tweet.

"Sijazungumza na Mbowe lakini nime-tweet ila nitazungumza naye. Hatua ya kwanza niliyofanya ni kupiga kelele kwa sababu hata mara ya kwanza nilifanya hivyo, lakini haikupita muda," alisema.

**ACHUKUA FOMU**

Jana asubuhi, Lissu akiwa na wasaidizi wake alifika ofisi za CHADEMA zilizoko Mikocheni, Dar es Salaam na kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa chama hicho.

Akizungumza baada ya kuchukua fomu hiyo, Lissu alisema endapo atachaguliwa atataka Tanzania ambayo watu wanaopenda haki.

"Kwa kuwa wenye haki wakiwa na mamlaka watu hufurahi na waovu wakitawala, watu huugua. Nataka uenyekiti wangu uwe ni kwa ajili ya kuhakikisha Tanzania yenye haki itakayoinua taifa letu na kufanya watu wetu wafurahi," alisema.

Lissu alisema licha ya kujitokeza kwa kundi la wafuasi wake kutaka kugharamia fomu yake ya kugombea nafasi hiyo, lakini amechagua ilipiwe na mwanachama aitwaye Edgar Mwakalebela (Sativa).

"Hizi fomu zinatakiwa zilipiwe ada yake ya Sh.1,500,000 ningeilipia mimi mwenyewe, lakini kuna wanachama wema wanaofikiri kama mimi, wanaofikiri kwamba uchaguzi huu uwe mwanzo mpya kwa ajili ya chama chetu, ambao wamechanga fedha kwa ajili ya kulipita gharama hii.

**Imeandaliwa na Elizabeth Zaya na Romana Mallya**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email:customerrelations@guardian*

HABARI KITAIFA

## Toto Afya Kadi rasmi na vifurushi vyake

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Afya, Jenista Mhagama amezindua mifumo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mpango wa Toto Afya Kadi ambao unaruhusu mtoto mmoja kujiunga kwa hiari kuanzia Sh. 150,000.

Katika mpango huo, NHIF umefanya mapitio ya fao hilo ili liwe endelevu na stahimilivu na kwa watoto watakaoandikishwa kupitia makundi yao ya shule watachangia Sh. 50,400 kwa mwaka.

Watoto watakaojiunga kwa utaratibu wa hiyari katika chaguo la kwanza litakuwa Sh. 658,000, la pili ni Sh. 237,000 na la tatu watalipa Sh. 150,000.

Waziri Jenista alisema jijini hapa jana kuwa mpango huo awali pamoja na uzuri wake wa kusaidia wananchi ulisababisha hasara kwa kuwa kwenye kila Sh. 100 mtoto alitumia takribani Sh. 600.

"Niwapongeze kwa kuwa wasikivu na kufanyia kazi maoni kutoka kwa wananchi na wadau wengine kuhusu mpango wa usajili wa mtoto mmoja mmoja iwapo itatokea kwamba mtoto hayuko shuleni," alisema.

Hivyo, alitoa wito kwa wananchi kuwasajili watoto wao ili kuhudumiwa kwa utaratibu wa bima ya afya na kuhakikisha wanakuwa walinzi wa huduma ili mfuko usiibiwe kupitia huduma za watoto.

Kuhusu mifumo, alisema kuzinduliwa kwa mifumo hiyo ni mwarobaini wa vitendo vya udanganyifu vilivyokabili mfuko kwa muda mrefu.

Aliagiza maboresho ya mifumo yafanyike mara kwa mara kwa kuzingatia mazingira halisi na isizalishe tena changamoto ambazo zitaathiri uhai na uendelevu wa mfuko.

Kadhalika, aliagiza mfumo katika mchakato wa vifurushi mbalimbali vya kuwezesha wananchi kujiunga kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wahakikishe havina malalamiko ili kusaidia sekta ya afya kusimama vizuri.

Jenista alikemea tabia ya baadhi ya watoa huduma kutumia mfuko kujipatia mapato yasiyo halali kwa njia ya udanganyifu na kutaka mifumo hiyo ilindwe ili isiingiliwe na watu wajanja, isomane na taasisi nyingine na ipatikane hadi vijijini ili wananchi wapate huduma kwa urahisi.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dk. Irene Isaka alisema kwa watoto watakaojiunga kwa Sh. 150,000 kiwango cha ukomo watatumia Sh. 2,000,000 kwa wanaolazwa huku wagonjwa wa nje ni Sh. 1,000,000.

Alisema kwa watoto watakaojiunga kwa Sh. 237,000, wanaolazwa kiwango cha ukomo ni Sh. milioni nane na wagonjwa wa nje ni Sh. milioni mbili, huku kwa watakaolipa Sh. 658,000 kiwango cha ukomo ni Sh. milioni 22 na wagonjwa wa nje ni Sh. milioni tatu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, Elibariki Kingu alisema NHIF ni roho ya taifa kwa sababu ustahimilivu wake unaweza kusababisha amani na utulivu wa nchi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email:customerrelations@guardian*

# Makamu Rais Z'bar: Utitiri wa kodi na wasimamizi wengi vinawatesa walipaji

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Rais ya Maboresho ya Kodi imekutana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ili kujitambulisha.

Tume hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Balozi Ombeni Sefue na ujumbe wake, walijadili mambo mbalimbali ikiwamo mapendekezo yatakayozishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) kuhusu masuala ya kodi.

Akizungumza baada ya kuupokea ujumbe huo, Dk. Mwinyi alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiteua tume hiyo ambayo alisema itasaidia kuimarisha na kubadilisha mifumo ya kodi kwa serikali hizo na kuleta mageuzi kwenye biashara hususani eneo la kodi.

Wakati huo huo, Tume hiyo ilikutana na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman.

Othman, alitahadharisha kuwa mfumo wa kodi uliopo nchini unaruhusu utitiri wa kodi nyingi kusimamiwa na mamlaka tofauti na kuhatarisha kuanguka kwa biashara nchini.

Alisema kuwapo kwa mamlaka nyingi za kodi mbali na kusababisa usumbufu kwa wafanyabiashara nchini ni changamoto kubwa ambayo ni muhimu kwa tume hiyo kuangalia upya, hususani katika sekta ya uchumi ikiwamo usafiri wa anga na huduma katika sekta ya kilimo.

Alisema kuna haja kwa Tanzania kubadili mwelekeo wa mfumo wa kodi ndani ya nchi ili kurahisisha shughuli za kodi na biashara ili kwenda kwa wepesi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Aidha, licha ya taifa kujitahidi kukuza sekta mbalimbali ni vyema kuangalia mfumo sahihi wa kodi katika kilimo jambo litakalochangia rasilimali zilizomo kuwekezwa na kuleta tija ndani ya Tanzania.

Alisema hali ilivyo sasa inaweza kuchangia baadhi ya wafanyabiashara kushindwa sio tu kulipa kodi kikamilifu na nchi ikapata tija, lakini kutoendelea na shughuli za kibiashara jambo linalohitaji kuangaliwa kwa makini.

Akizungumzia suala la kodi katika sekta ya usafirishaji wa anga, Othman alisema Tanzania imeshawahi kuwa na kampuni nyingi ambazo zinatoa fursa nyingi za ajira, lakini bado ni eneo linalohitaji kurekebishwa zaidi katika mfumo wa kodi ili kusaidia tija zaidi kwa manufaa ya nchi.

Alisema kutokana na hali hiyo hivi sasa, usafiri wa anga umekuwa ni biashara na huduma inayoweza kutumiwa na watu matajiri pekee jambo ambalo linahitaji kuangaliwa zaidi ili sekta hiyo ya anga iweze kukua zaidi.

Kadhalika, alishauri kwamba kutokana na mazingira ya Tanzania kunahitajika kuwapo mfumo wa kodi unaolenga hali halisi ya nchi ili kusaidia nchi katika kukusanya kodi na kuchangia ukuaji wa uchumi kama zinavyofanya nchi nyingine.

Pia, alishauri kuwapo na mamlaka chache za kodi ili kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kusimamiwa na taasisi nyingi za kodi jambo litakalochangia kukua kwa biashara ndani ya nchini.

Mwenyekiti wa tume hiyo, Balozi Ombeni Sefue, alisema kwamba imepewa jukumu la kukutana na wadau ili kuangalia mfumo wote wa kodi na kuwasilisha serikalini mapendekezo ya kuboresha mfumo wa kodi Tanzania.

Alisema kwamba hatua hiyo ni kuisaidia serikali kufanya marekebisho na kuufanya mfumo wa kodi ulipo nchini kuwa rahisi na kuweka mazingira mazuri ya kibiashara Tanzania.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha (kulia), akisalimiana na Mkuu wa Majeshi, CDF Michael Mkenda, jana alipofika kwa ajili ya kumsalimia na kujadili mambo mbalimbali yahusuyo kazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Msajili wa Vyama John Tendwa afariki dunia

**Na Halfani Chusi**

MSAJILI wa Vyama vya Siasa mstaafu, John Tendwa amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alikokuwa anapatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, Tendwa alifikwa na umauti usiku wa kuamkia jana. Msiba uko nyumbani kwa marehemu Kibamba Hospitali, Dar es Salaam na taratibu za mazishi zinaendelea kuratibiwa na familia kwa kushirikiana na ofisi yake.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, mtoto wa marehemu, Willium Tendwa alisema baba yake alifariki usiku wa kuamkia jana na kwamba taratibu za mazishi zitatangazwa baada ya familia kukaa na kukubaliana.

"Tunasubiri watoto wengine wafike jioni ya leo (jana) ili tuweze kukubaliana pamoja na kupanga ratiba za maziko," alisema Willium.

Kwa mujibu wa Wilium, baba yao ameacha watoto wanane (wa kike wanne).

Tendwa alitumikia nafasi hiyo kwa miaka 13 kuanzia mwaka 2001 hadi 2013, akipokea kijiti kutoka kwa mtangulizi wake, George Liundi kisha kumwachia Jaji Francis Mutungi ambaye anaongoza hadi sasa ofisi hiyo.

Tendwa atakumbukwa kauli yake aliyowahi kuitoa enzi za uhai wake akiwa madarakani kwamba vyama vya siasa vitakavyobainika kusababisha mauaji vitafutiwa usajili kutokana na kukiuka sheria, kanuni na utaratibu wa uendeshaji shughuli za siasa nchini.



Skani hapa kutembelea chaneli yetu

RIPOTI MAALUMU -3

# Kilichokutwa shule jirani na makaburi kinavyokinzana na maelekezo serikalini

**Na Mwandishi Wetu aliyekuwa**
MBINGA

**KATIKA sehemu ya tatu ya ripoti hii jana, kulikuwa na ushuhuda wa miundombinu chakavu shuleni Lipumba, wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma. Endelea na sehemu ya mwisho kupata undani wa mustakabali wake.**

---

HAKUNA utafiti rasmi uliofanyika shuleni Lipumba kubaini madhara ya madarasa kujengwa karibu na makaburi na athari za uhaba na uchakavu wa miundombinu shuleni huko.

Hata hivyo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, katika ripoti yake ya mwaka 2020/21, anabainisha kuwa uhaba na uchakavu wa miundombinu shuleni ni miongoni mwa sababu zinazochangia ufaulu duni wa wanafunzi wa shule za msingi nchini.

Ufuatiliaji wa mwandishi wa habari hii kuhusu mwenendo wa kitaaluma shuleni Lipumba, umebaini shule hiyo haifanyi vizuri kitaaluma.

Matokeo ya mitihani ya taifa, ambayo kitaaluma na kiserikali ndio nyenzo halisi ya kufanya tathmini kilichovunwa katika uwekezaji huo, yanaonesha shule hii ina tatizo.

Kwa mujibu wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), kwa miaka minne kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, hakuna mwanafunzi kutoka Lipumba aliyefaulu kwa daraja "A". Hata wanaofaulu kwa daraja "B" ni wachache.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **2024** | | | | | |
| Jinsi | A | B | C | D | E |
| Ke | 0 | 3 | 9 | 9 | 0 |
| Me | 0 | 0 | 4 | 5 | 1 |
| Jumla | 0 | 3 | 13 | 14 | 1 |
| **2023** | | | | | |
| Jinsi | A | B | C | D | E |
| Ke | 0 | 9 | 18 | 12 | 1 |
| Me | 0 | 2 | 13 | 11 | 0 |
| Jumla | 0 | 11 | 31 | 23 | 1 |
| **2022** | | | | | |
| Jinsi | A | B | C | D | E |
| Ke | 0 | 4 | 34 | 24 | 0 |
| Me | 0 | 5 | 40 | 34 | 0 |
| Jumla | 0 | 9 | 74 | 58 | 0 |
| **2021** | | | | | |
| Jinsi | A | B | C | D | E |
| Ke | 0 | 17 | 11 | 4 | 0 |
| Me | 0 | 10 | 12 | 8 | 1 |
| Jumla | 0 | 27 | 23 | 12 | 1 |

Mchanganuo wa matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Upimaji Darasa la Saba kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 katika Shule ya Msingi Lipumba. **CHANZO: NECTA.**

Kinachoshuhudiwa katika Shule ya Msingi Lipumba pia kinakinzana na miongozo ya kitaifa kielimu, ikiwamo Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inayoitegemea sekta ya elimu, ambayo 'karakana' yake mojawapo ni shuleni Lipumba, iisaidie.

Dira hiyo inaipa jukumu Sekta ya Elimu na Mafunzo kunoa rasilimaliwatu kitaifa ili kuwa na watanzania mahiri walioelimika ili kuliletea taifa maendeleo endelevu na kuliweka kwenye uchumi shindani duniani.

Hali ya miundombinu shuleni Lipumba pia ni ishara ya kutofanyiwa kazi mapendekezo ya CAG aliyoyatoa kwa serikali miaka saba iliyopita.

Katika Ripoti ya Ukaguzi Maalumu wa Miundombinu na Samani kwenye Shule za Msingi Tanzania aliyoitoa Machi 2017, CAG (kipindi hicho Prof. Mussa Assad), anasema alibaini hali mbaya ya miundombinu na samani katika shule zinazomilikiwa na serikali.

Huku akidokeza kuwapo ongezeko la wanafunzi kwa wastani wa asilimia tano kila mwaka, CAG Assad alitoa mapendekezo ya maboresho, kwamba "serikali ichukue hatua za haraka kuboresha miundombinu iliyopo na kujenga mipya".

Ni uhalisia unaopata uthibitisho katika ripoti ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, ambamo CAG wa sasa, Charles Kichere, anasema ufuatiliaji wa utekelezaji mapendekezo ya Ripoti ya Ukaguzi Maalumu wa Mwaka 2017, umebaini "serikali inasuasua".

CAG Kichere anafafanua kuwa katika halmashauri 48 alizokagua, ikiwamo ya Mbinga iliko Shule ya Msingi Lipumba, amebaini uboreshaji miundombinu unasuasua.

"Kwa kuzingatia uchambuzi huu, ni wazi kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hawakutekeleza kikamilifu mapendekezo yangu ya mwaka 2017.

"Hii inaweza kuwa miongoni mwa sababu zinazochangia ufaulu duni wa wanafunzi wa shule za msingi nchini. Hali hii inadidimiza juhudi za serikali katika kuboresha elimu ya msingi na sekondari," CAG Kichere anabainisha.

Anapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wafanye tathmini kuhusu dosari alizozibaini ili kuboresha elimu ya msingi.

Hata hivyo, CAG Kichere ana angalizo kwamba, hilo litawezekana ikiwa Hazina itatoa fedha za kutosha na kuweka mikakati inayotekelezeka ili kukabiliana na dosari zilizobainika.

Kwa tathmini ya haraka, wanafunzi waliojiunga na elimu ya msingi mwaka 2017 baada ya ripoti hiyo ya CAG kutolewa, ndiyo wahitimu wa darasa la saba mwaka huu, ambao juzi walipangiwa shule za kujiunga kidato cha kwanza mwakani.

Katika kipindi hicho cha miaka saba, hali mbaya ya miundombinu shuleni Lipumba haijapata mageuzi stahiki. Hata kidogo kinachofanyika sasa shuleni ni juhudi za wanakijiji kukabili magumu yao kwa ujenzi wa vyoo na darasa. Serikali inaendelea na ujenzi wa darasa moja ndani ya miaka saba ya utekelezaji hoja ya CAG.

Wakati Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Joseph Kashushura akitoa ufafanuzi kuwa hana bajeti ya kutosha kutatua matatizo hayo ya Lipumba na shule nyinginezo zilizomo katika himaya yake, taarifa rasmi za kiserikali zinaonesha kupotea mabilioni ya shilingi ambayo yangetumika kuboresha miundombinu shuleni.

Mtazamo huo wa fedha za umma kufanyiwa ubadhirifu, hata kusababisha pengo la ufanisi kwenye huduma za umma, unawasilishwa kupitia Uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23 uliofanywa na taasisi ya WAJIBU.

Kwa mujibu wa WAJIBU, chombo kinachosimamiwa na CAG mstaafu Ludovick Utouh, mwanazuoni wa uhasibu, imebainika miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, inayofikia Sh. trilioni 11.857 ndani ya miaka minne (2019/20 - 2022/23).

Hapo panatolewa ufafanuzi namna Sekta ya Elimu inaathirika kwa tafsiri: "Kiasi hicho kama kingeelekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kingetosha kujenga vyumba vya madarasa mpya 592,850.

"Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote."

Kimsingi, uhaba wa miundombinu na samani shuleni Lipumba na kwingineko nchini, unakwaza utekelezaji Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26).

Katika Sekta ya Elimu, mpango huo unaelekeza ifikapo mwaka 2026, mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari yawe yameboreshwa kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa na ununuzi wa madawati.

Hali kadhalika, unagusa kuboreshwa uwiano wa vyoo na mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote na makazi yao kuwa karibu na maeneo ya kazi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email:customerrelations@guardian*



Sehemu ya makaburi ya kijiji jirani na madarasa ya Shule ya Msingi Lipumba

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77/- | Bil 770.91/- | Bil 676.66/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/ | Bil 297.86/- | Bil 499.96/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36/- | Bil 2,015.78/- | Bil 1,234.67/- |
| Jumla | Bil 1,770.84/- | Bil 4,590.73/- | Bil 3,084,55/- | Bil 2,411.29 |

Mwenendo wa viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23. **CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya Taasisi ya WAJIBU Mei 2024. Uk. 4**



Moja ya nyumba za walimu shuleni Lipumba

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# INATANGAZWA TENA: MAOMBI YA KUONESHA NIA: UTOAJI MSAADA WA HUDUMA YA MANUNUZI, UGAVI NA USAFIRISHAJI WA VIPURI VYA MATENGENEZO, NA VIFAA VINGINE VYA MATUMIZI YA AWALI KWA AJILI YA EACOP: KUMBUKUMBU NA. REQ-00000659

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD ("EACOP LTD") linakaribisha kampuni yenye uzoefu na weledi wakutosha kuonesha nia ya kutoa Msaada wa Huduma ya Manunuzi, Ugavi na Usafirishaji wa Vipuri vya matengenezo, na vifaa vingine vya matumizi ya awali kwa ajili ya EACOP kwa ajili mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi linalovuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya kimataifa. Bomba hilo litaanzia Kabaale wilayani Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania. Bomba hilo litapita katika mikoa minane (8) inayojumuisha Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga, Halmashauri za Wilaya 27 za Tawala na Vijiji 231.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) utahitaji suluhisho Madhubuti ili kusaidia utayari wake wa utendaji wa shughuli katika Kituo cha Kuhifadhia Mafuta Baharini (MST), Tanga, Tanzania. Huduma hii inapaswa kujumuishavipengele vifuatavyo.

Kamasehemu ya dhamira ya kampuni ya kukuza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa Raia wa Tanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, EACOP inatafuta huduma za makampuni yanayotambulika na yenye sifa na uzoefu wa kutoa huduma za manunuzi kwa ajili ya ununuzi na usafirishaji wa vipuri kwa ajili ya matengenezo na manunuzi vifaa vya awali vya matumizi ili kusaidia Uendeshaji wa shughuli katika eneo la kazi. Kulingana na orodha ya vipuri iliyotolewa na mkandarasimkaguzi wa uhandisi, mtoa huduma atasimamia:

- Mchakato wa manunuzi,
- Vifaa na huduma zinazohusiana na maombi au oda iliyotolewa,
- Utoaji wa eneo la kuhifadhia na
- Kuwasilisha kwenye ghala la EACOP la kituo cha Tanga na kuingiza data/taarifa husika kwenye mfumo wa KAMPUNI.

Malengo ya EOI hii ni kutafuta mkandarasi anayeweza kutoa huduma Madhubuti ya ununuzi na usafirishaji ili kusaidia utoaji wa huduma ya matengenezo, unaojumuisha aina mbalimbali za kazi muhimu, ikiwa ni pamoja na:

**USIMAMIZI WA NYARAKA**
- Usimamizi wanyaraka za mzabuni, vyeti , na rekodi au taarifa zinazohusiana.

**HUDUMA ZA MANUNUZI**
- Utayarishaji wa Mkataba na /au agizo la Ununuzi, mapitio ya zabuni, ufafanuzi, tathmini na masuala ya mapendekezo.
- Usimamizi kamili wa manunuzi, ikijumuisha usambazaji wa vifaa, zana na vipuri muhimu.
- Utoaji wa vipuri na vifaa vya matumizi kwa ajili ya uendeshaji wa awali na matengenezo yanayoendelea ya mtambo.
- Usimamizi Madhubuti wa mikataba na viambatishi vyake

**HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**
- Usafirishaji na utunzaji wa mizigo hadi mwisho.
- Upakiaji, ufungaji, upakuaji na upangaji wa mzigo.
- Ushughulikiaji wa mizigo na Usaidizi wa kutoa mizigo ya wateja bandarini
- Uhifadhi wa mizigo inayoingia.
- Usimamizi wa Leseni zinazohitajika za uagizaji mizigo (ikijumuisha nyaraka za uagizaji bidhaa, PVoC, GCLA n.k.).
- Mfumo wa usimamizi wa ghala ili kuhakikisha uhifadhi ulioboreshwa.

**HUDUMA ZINAZOHITAJIKA**
- Ukusanyiko wa vifaa kutoka eneo kwa mzabuni.
- Usafirishajiwa baharini na nchi kavu (ikiwa ni pamoja na usafirishaji wa ndani ya nchi).
- Masharti ya dhamana ya Usafirishaji: kutoka kwa DAP mpaka kwenye maghala ya kampuni katikaVituo vya Baharini, Tanga.
- Ukaguzi, upimaji, na usimamizi wa bima.

**KUHIFADHI, KUTUNZA, KULINDA**
- Utoaji wa miundombinu ya kuhifadhia ya muda kama inavyohitajika.

**UCHAKATAJI WA DATA MAPOKEZI**
- Usajili wa bidhaa zilizopokewa ndani ya mfumo wa ERP wa KAMPUNI.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi kwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo:
- Maelezo mafupi yanayoonesha uzoefu wa kufanya shughuli kama hizo.
- Uzoefu bayana wa kufanya shughuli kama hizo kwa ufanisi katika usaidia wa miradi mikubwa.
- Uthibitisho wa uzoefu wa angalau miaka 6 katika kutoa huduma sawa hii kwa miradi au makampuni yanayohusiana ikijumuisha barua za uthibitisho kutoka kwa wateja watatu wa hivi karibuni .
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi cha mwaka huu. (Ambatanisha nakala).
- Nakala ya ripoti rasmi ya Kampuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni toka BRELA. (Ambatanisha nakala).
- Cheti cha usajili na leseni ya Biashara. (Ambatanisha nakala).
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Wasifu wa watendaji wakuuwatakaohusika katika utoaji wa Huduma ikiwa ni pamoja na vyeti vyao, kiwango cha uhitimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika katika miradi mikubwa.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana nasera za kupinga rushwa, ufisadi, naSera YA Haki za Binandamu.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha wamesajiliwa au kuonesha uthibitisho wa maombi ya kujisajili kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani.

---

Makampuni yenye nia na uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hao juu yanapaswa kuonesha nia yao kwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwenda **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb). Maombi yatumwe kabla au saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), kabla au tarehe ya **15/1/2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000659 – Utoaji Msaada wa Huduma ya Manunuzi, Ugavi na Usafirishaji wa Vipuri vya matengenezo, na vifaa vingine vya matumizi ya awali kwa ajili ya EACOP.** Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.**Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.**

---

**Muhimu**: Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

182998

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Hatua kali zichukuliwe dhidi ya ubadhirifu fedha za umma*

**MARA** kwa mara kumekuwa na taarifa za ufujaji na wizi wa mabilioni ya shilingi katika taasisi na idara za serikali unaofanywa na baadhi ya watendaji waliopewa dhamana ya kusimamia fedha hizo kwa ajili ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

Taarifa hizo zimekuwa zikibainisha kwamba fedha hizo zinazopigwa na watendaji hao ni zile zinazotolewa na serikali kuu na za mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama vile ya elimu, afya na miundombinu.

Fedha zingine ni zile zinazotokana na ukusanyaji wa ushuru katika minada, masoko na mialo na ubadhirifu huo hufanya na watendaji wa halmashauri kwa kushirikiana na wazabuni.

Ubadhirifu au upigaji wa fedha za umma umekuwa ukidaiwa kufanywa na watendaji wa taasisi kwa kushirikiana na wazabuni. Katika eneo hilo, baadhi ya zabuni hutolewa kwa misingi ya upendeleo lengo likiwa kujipatia chochote kupitia fedha za utekelezaji wa kazi mbalimbali kama ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, maji na elimu.

Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Kamati za Kudumu za Bunge, Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) zimekuwa zikibainisha mara kwa mara upigaji unaofanywa na watendaji hao. Ripoti hizo zimekuwa zikijirudia kila mwaka lakini hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa ili kukomesha vitendo hivyo visiendelee.

Aidha, kila viongozi wakuu wa serikali, kwa maana ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu wanapofanya ziara katika mikoa kukagua shughuli za maendeleo, wamekuwa wakikutana na madudu hayo ambayo yamesababisha mabilioni ya fedha za umma kuingia katika mifuko ya wajanja wachache.

Matokeo ya kuendelea kwa vitendo hivyo ni kukithiri kwa ubadhirifu wa fedha za umma na hatimaye kuzorotesha miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa mantiki hiyo, kero zinazowakabili wananchi zimekuwa zikiendelea kuwapo huku yakitolewa maagizo ya kusimamishwa kazi kwa watuhumiwa ili kupisha uchunguzi kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pamoja na kuwapo kwa ushauri wa CAG kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya waliohusika na ubadhirifu pamoja na maagizo yanayotolewa na viongozi hao, utekelezaji wa hatua hizo ikiwamo uchunguzi wa TAKUKURU, hatua zinazochukuliwa hazikidhi kiu ya wananchi kuona wahusika wanafikishwa katika vyombo vya sheria na kuadhibiwa.

Kuwapo kwa hali hiyo, kunafanya misamiati ya ubadhirifu, wizi na upigaji kuwa kama aya ndani ya misahafu na kuwafanya baadhi ya watumishi pia kuona ni mfumo wa kawaida ulioko katika maisha, hivyo wapigaji wa mabilioni hayo kuonekana ndio mashujaa na wale wanaofuata maadili kuwa kama waliozubaa.

Kuibuliwa kwa madudu hayo, ni dhahiri kwamba chanzo kikuu ni kukosekana kwa usimamizi imara wa fedha hizo unaopaswa kufanywa na wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na watendaji wakuu wa wizara. Kwa hali ya kinadharia, kuendelea kwa hali hiyo kunaweza kuitafsiriwa kuwa kuna mnyororo wa ushirikiano katika ngazi mbalimbali ambao pia kusababisha watu kulindana.

Maneno na hadithi za upigaji mabilioni ya fedha za hauna budi kufika mwisho kwa serikali kuchukua hatua. Njia inayoweza kufanikisha hilo ni kuimarisha uwajibikaji kwa watendaji.


Iwapo kutatokea ubadhirifu katika sekta fulani na sehemu husika, waliohusika wakawajibishwa sambamba na mkuu wa wilaya, mkurugenzi wa halmashauri, katibu tawala wa mikoa na hata waziri wa kisekta, ni wazi kwamba kila mtu atajifunza kusimamia mali za umma kwa kuhofia kupoteza kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# *Undugu huu ni tishio abiria*

Na Tuntule Swebe

**MAKONDAKTA** wa daladala inavyoonekana ni marafiki wakubwa wa wapigadebe waliopo kwenye vituo mbalimbali vya mabasi.

Ni kutokana na ukweli kwamba wengi wa makondakta hao ni zao au wametoka kwenye kundi hilo.

Ushirika huo umejenga urafiki kati ya makundi hayo mawili na hupeana kazi ya kupiga debe, kwa ajili ya kujaza abiria ndani ya daladala kwenye vituo vya mabasi mikoani na majijini na kupewa ujira wa shilingi 200 hadi 500.

Hata hivyo, baadhi ya wapigadebe wanatuhumiwa kujihusisha na tabia ya kuwachomolea fedha abiria na inawezekana hata vitendo hivyo hufanyika huku makondakta wakijua.

Kuwanyamazia wezi hao kunatokana na ukweli kwamba ni marafiki zao wa karibu wanaopeana kazi ili mkono uende kinywani. Lakini ni vyema wakatambua kuwa wanaharibu kazi yao.

Mtindo huo si mpya bali ni wa muda mrefu, lakini sina budi kukumbusha kuwa inatosha kuwalea watu wa aina hiyo kwa kuwapa kiasi hicho cha fedha ambacho kimsingi hakitoshi kuendesha maisha.

Jambo la muhimu ni kusaidiana kutafuta kazi halali ambazo zitawasaidia kuendesha maisha badala ya kujificha chini ya mwamvuli wa upigadebe huku wakiwaibia abiria ndani ya daladala.

Inasikitisha kuona kijana mwenye nguvu zake anashinda katika kituo cha daladala na kufanya kazi ya kuibia abiria badala ya kutumia nguvu hizo kufanya kazi halali kwa ajili ya maisha ya baadaye.

Muda ambao abiria wamekuwa wakiibiwa ni asubuhi wanapokwenda kazini na hata jioni wanaporejea majumbani, kutokana na kwamba ndio wakati ambao daladala nyingi huwa zimejaa abiria.

Kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo ambavyo pia uhusisha vibaka wengine, ingekuwa ni vyema sasa kazi ya ukondakta ikawa ni kazi rasmi inayoheshimiwa badala ya kuwa na watu wa ziada.

Yaani madereva na makondakta waajiriwe ili kuondoa sintofahamu hiyo, kwani wakiwa katika ajira, haitakuwa rahisi kuruhusu wapigadebe kuwasaidia kufanya kazi ya kuita abiria.

Kuwapo kwa wapigadebe kunatokana na uholela wa kazi hiyo, lakini kama wahusika wataajiriwa, itakuwa ni rahisi kufanya kazi yao kwa umakini bila kuruhusu wapigadebe kuwasogelea.

Uholela wa kazi hiyo umesababisha karibu vituo vyote vya daladala hasa jijini Dar es Salaam kujaa wapigadebe ambao wanajificha chini ya mwamvuli wa upigadebe lakini wakijihusisha pia na wizi.

Ninaamini katika mazingira hayo, itabidi wapigadebe watafute kazi nyingine halali ya kufanya badala ya kuhangaika na shughuli ambazo hazina manufaa yao ya baadaye.

Sio vibaya wakajiunga katika vikundi na kupata mkopo wa fedha zitakazowawezesha kuanzisha biashara ili waweze kujikimu kimaisha kuliko kuhangaika na vitu ambavyo havina manufaa kwao.

Vilevile, umefika pia wakati wa kuacha mtindo wa kurundika abiria ndani ya daladala kama mizigo, kitendo ambacho ni hatari kwani kinaweza kusababisha wakaambukizana magonjwa.

Ingependeza kama askari wa kikosi cha usalama barabarani wakalisimamia hilo, ili kila daladala ibebe abiria na kuwaachia nafasi ya kupumua hata kama kuna changamoto ya usafiri.

Ninajua kuwa katika jiji la Dar es Salaam, kuna changamoto ya ukosefu wa usafiri wa kutosha wa daladala, lakini hilo lisiwe kigezo cha kurundika abiria ndani kupita kiasi.

Ikumbukwe kuwa vijana ndio taifa la kesho linalotegemewa kuisaidia nchi, hivyo wasiachwe katika mazingira hayo ambayo yatawafanya wawe taifa la kesho lisilo na umuhimu ndani ya jamii.

Zipo njia mbalimbali nilizotaja za kuwasaidia wapigadebe hao, lakini pia makondakta wenyewe wajaribu kupunguza urafiki na kundi hilo ili kulinda heshima ya kazi yao mbele ya abiria.

**Ninajua kuwa katika jiji la Dar es Salaam, kuna changamoto ya ukosefu wa usafiri wa kutosha wa daladala, lakini hilo lisiwe kigezo cha kurundika abiria ndani kupita kiasi.**

## Mtuhumiwa uporaji adaiwa kufariki dunia kwenye mapambano na polisi

**Na Julieth Mkireri**

RAMADHANI Juma (22) anadaiwa kufariki dunia katika mapambano na polisi waliotaka kumkamata kwa tuhuma za kuhusika na tukio la wizi huku mmoja wa askari akijeruhiwa kichwani kwa panga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase amesema tukio hilo lilitokea Desemba 15 mwaka huu baada ya Juma na wenzake kudaiwa kupora simu na begi lenye vitu mbalimbali, mali ya Fortunatus Matutu.

Akielezea tukio hilo, Kamanda Morcase alidai kuwa Desemba 15, saa 10:40 alfajiri, Matutu akiwa anaelekea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi), gari lake lilipata hitilafu maeneo ya TAMCO na kulazimika kushuka kufanya marekebisho.

Alisema kuwa akiwa kwenye marekebisho ya gari lake, ghafla walitokea vijana watatu wakiwa kwenye pikipiki aina ya boxer nyeusi yenye namba za usajili MC 429 DPV ambao walimshambulia kwa mapanga Matutu sehemu mbalimbali za mwili kisha kumpora mali hizo.

Kamanda huyo alieleza kwamba baada ya kupata taarifa za tukio hilo, walianza kufuatilia na kufika eneo ambalo watuhumiwa hao walikimbilia na wakiwa wanajaribu kuwakamata ndipo Juma alimshambulia askari D/CPL DERICK kwa kumkata na panga kichwani na kumsababishia jeraha.

Watuhumiwa hao walianza kukimbilia eneo ambalo askari walitoa onyo na amri kusimama, lakini walikaidi na kuendelea kukimbia ndipo mmoja wao ambaye ni Juma alipigwa risasi ya paja la kulia na mkono wa kulia kufanikisha ukamataji.

"Hata hivyo, mtuhumiwa huyo kutokana na majeraha aliyopata na kusababisha damu kuvuja kwa wingi, alifariki dunia akiwa njiani kwenda kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa, Tumbi.

"Mwili wa marehemu Ramadhani umehifadhiwa Hospitali ya Tumbi kwa uchunguzi wa daktari na askari aliyejeruhiwa aliruhusiwa baada ya kupata matibabu," alisema.

Kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi linaendelea na msako kuwakamata watuhumiwa walioshirikiana na Juma katika tukio hilo la unyang' anyi kwa kutumia silaha.

Kamanda huyo alidai Juma ni miongoni mwa vijana wanane waliokuwa tishio kwa uporaji. Sita kati yao wameshakamatwa na mmoja anaendelea kutafutwa pamoja na wanaoshirikiana nao.



Wakulima wa zao la korosho Chama Kikuu cha Ushirika Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU) mkoani Mtwara wakifuatilia mnada wa zao la korosho uliofanyika mwishoni mwa wiki wilayani Masasi mkoani Mtwara. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Waziri aagiza utatuzi wa sintofahamu ya mipaka mradi mabasi yaendayo haraka

**Na Ally Hengo**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi amemwagiza mtendaji mkuu wa mradi wa mabasi yaendayo haraka, maarufu mwendokasi, kufika eneo la makazi ya wananchi wa Kunduchi Mtongani, manispaa ya Kinondoni ili kuondokana na sintofahamu ya mipaka kuhusiana na mradi huo kutwaa eneo.

Agizo la waziri huyo lilitolewa mbele ya wananchi hao ambao kabla ya hapo walimwuliza swali Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima kuhusiana na kuwapo mradi huo unaohusisha zaidi ya nyumba 200 huku taarifa nyingine zikitoa takwimu tofauti.

Baada ya kuulizwa swali hilo, Mbunge Gwajima alimpigia simu Waziri Ndejembi na kumweka sauti ya juu ili uamuzi wake usikilizwe na wananchi hao na kuwaomba wampe dakika chache awasiliane na Mtendaji Mkuu wa mradi huo ili awape majibu sahihi.

Mtendaji huyo, Dk. Athumani Kihamia alipopatikana kwa njia hiyohiyo ya simu, alimwahidi Mbunge Gwajima kuwa ili kuondoa sintofahamu hiyo, atakwenda mwenyewe na watendaji wake na kupita katika mitaa yote leo ili kuonesha mipaka. Baada ya hapo kila mmoja atafahamu kama yumo ndani ya mradi au la.

Hata hivyo, wananchi hao walisema hawako radhi kuondoka katika maeneo hayo walimoishi kwa zaidi ya miaka 20 wakiwa wamiliki kihalali.

**Hata hivyo, wananchi hao walisema hawako radhi kuondoka katika maeneo hayo walimoishi kwa zaidi ya miaka 20 wakiwa wamiliki kihalali.**

Mmoja wa wananchi hao, Karita Mdoe alisema hawapingi mradi kama una manufaa kwa nchi, lakini ipo haja kuchukua maeneo mengine yaliyo wazi kama eneo wanalopakana nalo ambalo linamilikiwa na manispaa ya Kinondoni. Walidai limeachwa bila matumizi kwa muda mrefu.

Wananchi hao walioonekana kuwa na hasira, walimwondoa mbele ya mbunge mkazi mwenzao aliyejitambulisha kwa jina la Suleiman Lwilo baada ya kutoa hoja, akiomba waondolewe na kulipwa fidia. Ni hoja iliyoonekana kuwakera.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Waziri aonya TLS matamko ya kisiasa

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro ameonya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kuhusu matamko ambayo yamekuwa yanatolewa na baadhi ya viongozi wake yenye msukumo wa kisiasa.

Dk. Ndumbaro alitoa onyo hilo wakati wa kutia saini makubaliano kati ya serikali na TLS katika masuala mbalimbali yaliyofanyika Mtumba jijini hapa.

Pasi na kutaja majina, waziri huyo alisema kuna baadhi ya viongozi wa chama hicho wamekuwa wanatoa matamko huku baadhi yakiwa na msukumo wa kisiasa na si kitaaluma.

Alisema "kuna wakati unakuta chama cha siasa kinatoa kauli dhidi ya serikali na baadhi ya viongozi wa TLS nao wanakuja mbele ya vyombo vya habari kutoa kauli hiyohiyo dhidi ya serikali, maana yake hawa wote wako pamoja".

Aliwataka TLS kutumia taaluma yao kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi kama ilivyoelekeza katiba yao.

Waziri Ndumbaro alisema chama hicho kinatakiwa kutoa ushauri kwa njia bora zaidi huku wakizingatia taaluma zao.

Alisema kuwa duniani kote hakuna serikali inayokubali kushushiwa heshima huku akisisitiza TLS kuzingatia miiko na maadili ya chama chao.

Dk. Ndumbaro pia alisema hivi sasa serikali inaendelea kutoa msaada wa kisheria kupitia kampeni ya msaada wa kisheria ambayo imeshafika katika mikoa 11, ikiwa na lengo la kufika nchi nzima.

Alisema TLS ni kiungo muhimu katika kampeni hiyo kwa sababu katika baadhi ya maeneo waliyopita wako wanachama wa chama hicho ambao wameshiriki.

Aliongeza kuwa TLS wanatakiwa kufanya kazi kwa karibu na serikali kwa sababu wote wanafanya kazi ya kuwahudumia wananchi wa taifa.

Waziri huyo alisema serikali inatoa gari kwa ajili ya kusaidia shughuli mbalimbali za TLS nchini na lengo ni kuona chama hicho kinakuwa kama vyama vingine vya kitaaluma.

Pia alisema serikali ina mengi ya kushirikiana na chama hicho na makubaliano hayo ni ishara ya kufunguliwa milango ya kushirikiana kwa pamoja.

Awali Makamu wa Rais wa TLS, Laetitia Ntagazwa alisema chama hicho kimepewa jukumu la kushauri serikali, Bunge na kuwatetea wananchi.

Ntagazwa alisema kuwa ushirikiano ambao waliingia jana ni kwa ajili ya kuongeza tija kwa manufaa ya umma wa watanzania.

Makamu wa Rais huyo aliomba serikali kusaidia TLS ruzuku kwa lengo la kuendelea kuwafikishia wananchi wengi zaidi huduma ya msaada wa kisheria



Mkuu wa wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule akiongoza zoezi la upandaji miti 500 kwenye Shule ya Sekondari ya Mbweniteta. Miti hiyo imetolewa na kampuni ya Bayport ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kupanda miti 1,000,000 kuunga mkono juhudi za serikali kupitia mikakati na sera zake endelevu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCRA yakabidhi kompyuta kwa washindi wa hisabati

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekabidhi zawadi za kompyuta mpakato (laptop) kwa washindi watano wa shindano la Hisabati Afrika lililofanyika Agosti mwaka huu Afrika Kusini na kushirikisha nchi 25 za Afrika.

Shindano hilo linaratibiwa na Chama cha Hisabati Tanzania chini ya Mwenyekiti wake, Dk. Saidi Sima ambaye aliambatana na washiriki hao nchini Afrika ya Kusini.

Katika shindano la mwaka huu, Tanzania iliwakilishwa na wanafunzi kutoka vyuo vikuu na sekondari. Washiriki watano waliwakilisha nchi na kati ya hao wanne walishinda medali za shaba kwa kushika nafasi ya tatu katika matokeo ya jumla.

Katika kufanikisha ushiriki wa shindano hilo, TCRA ilidhamini ujumbe wa Tanzania kwa kutoa tiketi za safari na pia kuandaa makala mbalimbali kuhamasisha ushiriki kwa wanafunzi hususani wasichana.

Kati ya washindi watano waliopata medali, watatu ni wasichana, hatua inayotajwa imekuwa chachu ya kushawishi wasichana kupenda masomo ya sayansi.

Kwa kutambua umuhimu wa hisabati kwenye maendeleo ya nchi, hususani teknolojia na uchumi wa kidijiti, TCRA iliamua kuwapa zawadi washindi hao, kila mmoja akipatiwa kompyuta mpakato ili ziwasaidie kwenye masomo yao na pia kuchagiza wanafunzi wengine kujitokeza kushiriki mashindano ya namna hiyo pamoja na kusoma masomo ya sayansi.

Akikabidhi kompyuta hizo kwa mwakilishi wa washindi hao aliyeambatana na Mwenyekiti wa Chama cha Hisabati Tanzania na wakufunzi toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa TCRA, Rolf Kibaja alisema mamlaka hiyo inachangia juhudi za serikali katika kuinua uchumi wa kidijitali kwa kuwawezesha wanafunzi kupenda na kusoma masomo ya sayansi.

"Ni faraja kwa TCRA kuona tunaweza kushinda kimataifa, hii inatafsiri ushiriki wa kila mmoja kwenye safari ya kuelekea uchumi wa kidijiti," alisema.

Mwakilishi wa wanafunzi walioshinda tuzo hizo, Ambrose Rutashobya ambaye alipokea zawadi za kompyuta hizo kwa niaba ya washiriki wenzake, alishukuru TCRA kwa kuwawezesha kushiriki na kushindana, pia kuwajengea uwezo kupitia kompyuta hizo ambazo anaamini ni chachu kwao kuendelea kufanya vizuri zaidi.

"Tuishukuru TCRA kwa zawadi hizi na kutambua juhudi zetu na thamani ya somo la hisabati kwakuwa linalipa," alisema huku akiwashauri wanafunzi wengine nchini kujifunza kwa juhudi kwenye masomo yote, hasa hisabati.

Mwenyekiti wa Chama cha Hisabati Tanzania, Dk. Saidi Sima, alishukuru TCRA kwa kutoa zawadi hizo za kompyuta tano kwa washindi hao, akisisitiza umuhimu wa kompyuta hizo kwenye kuwasaidia wanafunzi hao kwenye masomo na kujifunza ubunifu mbalimbali utakaowawezesha kuleta majawabu ya kitaalamu.

Kuhusu ushiriki wa wasichana kwenye somo la hisabati, Dk. Agnela Mandia kutoka UDSM, alitoa wito kwa watoto wa kike kujifunza na kupenda somo la hisabati huku akiwapongeza washiriki wa kike watatu waliopata medali tatu kati ya nne zilizotolewa kwa washiriki wa Tanzania.

"Ninafahamu kuwa watoto wa kike wana uwezo wa kufanya hisabati na masomo ya sayansi vizuri, hivyo ninawasihi wasiogope kwa kuwa wana uwezo wa kufanya vizuri," alisema.

Mamlaka ya Mawasiliano TCRA imekuwa ikishiriki katika kuinua elimu nchini kwa kuwa kinara katika uanzishwaji klabu za kidijiti ambazo ni suluhisho kwa wanafunzi kuanzia ngazi ya awali mpaka vyuo vikuu.

Vilabu hivyo vinategemewa kutibu changamoto ya ufaulu wa masomo ya hisabati na sayansi kwa kuwajengea fursa za kushiriki, kubuni na kujifunza kwa pamoja na kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi, hisabati, uhandisi na TEHAMA.

## Wapatiwa mafunzo uandaaji vitalu vya thamani ya ardhi

Na Munir Shemweta, KILIMANJARO

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi nchini (LTIP) imetoa mafunzo kwa Wathamini na Warasimu Ramani kwa ajili ya uandaaji vitalu vya Thamani ya Ardhi (Valuation Block).

Mafunzo hayo ya siku tatu yalianza juzi na yanahusisha wataalamu wa fani ya uthamini na urasimu ramani kutoka ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na halmashauri zote za mkoa huo.

Mratibu wa mafunzo hayo ambaye ni Mthamini kutoka Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Baraka Mollel, alisema, lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha na kuwafundisha wathamini na warasimu ramani ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa kipindi hiki ambacho Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inaboresha mifumo yake na kuwa ya kidijitali.

Aidha, mafunzo hayo yanawafundisha wathamini na warasimu ramani namna ya kuandaa vitalu vya thamani ya ardhi ili kusaidia utekelezaji wa shughuli za uthamini kama vile rehani, uhamishaji milki na uthamani kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya serikali.

"Uandaaji vitalu vya thamani kwa wathamini na warasimu ramani utajumuishwa kwenye mfumo wa e-ardhi utakaowezesha ulipaji tozo mbalimbali ikiwamo kodi ya ardhi na tozo nyingine zitokanazo na thamani," alisema Mollel.

Alitaja faida ya Vitalu vya Thamani ya Ardhi (Valutaion Block) kuwa, ni kuiwezesha wizara katika makusanyo ya kodi ya ardhi, miamala mbalimbali ya uthamini pamoja na tozo nyingine kama vile tozo ya mbele na wanatoa mafunzo namna ya kuandaa vitalu na kuwaelekeza kuunganisha katika mfumo wa e-ardhi.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kilimanjaro, Rehema Jato, ameishukuru Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kuona umuhimu wa kuupa mkoa wake kipaumbele cha kupata mafunzo hayo aliyoyaeleza kuwa ni muhimu kwa wathamini na warasimu ramani katika mkoa huo.

"Tunajua kuwa mafunzo haya yataenda mikoa yote, lakini angalau sisi Kilimanjaro tumekuwa watu wa mwanzo mwanzo hivyo tuyatumie mafunzo haya katika kuongeza ujuzi na hatimaye kufikia malengo," alisema Rehema.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanza matumizi ya mifumo ya kidigitali (e-ardhi) na hivi karibuni waziri Deogratius Ndejembi wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Ardhi aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kutumia mifumo ya teknolojia katika maeneo ambayo mfumo huo umeanza kutumika.

Mfumo wa e-Ardhi umeanza kutumika kwenye maeneo mbalimbali nchini kama Dodoma, Arusha, Tabora katika Halmashauri ya Nzega, Pwani Halmashauri ya Chalinze pamoja na Manispaa ya Shinyanga na Kahama zilizopo Mkoa wa Shinyanga.



# Maofisa TAKUKURU wajichimbia kutathmini uchaguzi wa S/mitaa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAOFISA wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Nchini (TAKUKURU) wanafanya tathimini ya uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, uliofanyika nchini Novemba 27 mwaka huu na kujipanga kwa uchaguzi mkuu wa 2025.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Crispin Chalamila

jijini hapa wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa taasisi hiyo.

Mkutano huo wa siku nne unaohudhuriwa na maofisa hao 206, ulifunguliwa juzi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kwa kuzingatia tumetoka kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa hivi karibuni na tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka kesho, tutatumia pia mkutano huu kupitia na kutathimini yaliyojiri katika kipindi cha uchaguzi huu ili kuweza kujipanga vizuri kwa uchaguzi mkuu 2025," alisema Chalamila.

Akifungua mkutano huo, Dk. Mpango, aliagiza TAKUKURU kuifanyia kazi taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa taasisi 44 za umma zilizokaguliwa mwaka 2022/2023.

Alifafanua kuwa taarifa hiyo ya ukaguzi ya PPRA, inaonesha zabuni 15 zenye thamani ya Sh. bilioni 67.27 zimetolewa kwa kutumia maelezo ya zabuni yenye kubagua baadhi ya wazabuni.

"Wazabuni walichaguliwa na kupewa mikataba 25 yenye thamani ya shilingi bilioni 56.7 pasipo kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni," alisema.

Alisema majadiliano ya mikataba 23 ya taasisi saba, yenye thamani ya shilingi bilioni 64.5 yalifanyika bila kuwepo kwa mpango wa mahojiano.

"Lakini pia, mikataba 60 yenye thamani ya shilingi bilioni 54, ilisainiwa pasipo kuidhinishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG). Na mikataba 10 ya manunuzi kwenye taasisi tano, yenye thamani ya shilingi bilioni 7.48 iliongezewa muda bila kufuata utaratibu," alisema.




Mratibu wa mtandao wa vikundi vya wakulima na wafugaji Mkoa wa Manyara (MVIWAMA), Valentine Ngorika (katikati). akizungumza kuhusu mabadiliko ya tabianchi na mikakati ya kuimarisha usalama wa chakula kwenye mkutano wa mwaka uliofanyika mjini Babati, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Chanzo familia kupoteza mali chatajwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Asia Matauka, amesema chanzo cha familia nyingi kupoteza mali au kufa kwa biashara ni wanaume kuficha vitega uchumi.

Matauka, alisema idadi kubwa ya wanaume wa Kilimanjaro, wanafanya biashara na kumiliki miradi mingi, huku wengine wakishindwa hata kuwaelekeza wake zao wanavyolipa kodi Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Akizungumza katika mkutano mkuu wa 13 wa mwaka wa Shirika la kiraia la Tusonge CDO, Mrakibu Matauka alisema kuwa: "Baba una vitega uchumi chungu nzima, lakini hata mkeo havifahamu.

"Hata tu ile TRA unalipiaje mapato mama hajui. Tuige ndugu zetu Watanzania wenye asili ya India, wanafundisha watoto na mke kuhusu biashara zao zinavyokwenda, wanarithishana na wanafanikiwa sana katika maisha, uchumi.

...Ukifariki dunia, mtoto wala mke, hana elimu ya biashara, hazijui mali zako zote, anaendelezaje? Hivi kutakuwa na mwendelezo? Ndio pale tunasema marehemu aliondoka na mali zake. Kwani ni kweli, yeye si alishakufa? zile mali sasa ameenda nazo wapi? Ni kweli wale waliobaki wameshindwa kuzitendea haki, kuzisimamia, ndio maana mali au biashara zinakufa."

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Aginatha Rutazaa, akielezea lengo la mkutano huo, alisema pamoja na kwamba hawakuweza kufikia asilimia 100 ya kugusa kila hitaji la mwanajamii, wanajivunia kuweka mbegu ndani ya jamii.

"Tunapofanya kazi kwa jamii, kuna mambo mengi yanayotokea, ziko changamoto zinajitokeza ziko nje ya uwezo wako. Tunakaa hapa pamoja kwa ajili ya kutafakari, hivi mwaka huu 2024, tulitembeaje ndani ya jamii? Inawezekana kuna mahali tulileta makwazo, inawezekana kuna mahali tulifanya visivyo, inawezekana kuna mahali tungeweka mchakato tofauti kidogo matokeo yangekuwa mazuri zaidi.

Aliongeza kuwa: "Ukikaa kwenye kiti ulichokikalia kumbuka kuna watu 300 wako nyuma yako kama umetoka kwenye kata ambayo ina mradi ambao unaendelea sasa hivi.

"Tunakwenda mwaka mwingine wa mzunguko wa miradi yetu. Hatuwezi kuthubutu kama taasisi kufungua mlango wa kuingia kwenye mwaka mpya wa mradi kabla hatujakaa na wadau wetu."

## Siha walilia gari la zimamoto

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKAZI wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro, wameomba serikali kuwapatia gari la zimamoto ili kukabiliana na majanga kwenye makazi yao.

Wakazi hao walitoa ombi hilo kutokana na wilaya hiyo kukosa gari hilo na kulazimika kutumia kutoka Moshi mjini na kuchelewa kufika na kukuta mali zimeteketea.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi hao walisema kuna ulazima kwa wilaya yao kuwa na gari hilo kutokana na kukumbwa na majanga ya moto mara kwa mara.

"Wilaya haina gari la zimamoto, moto ukizuka inabidi gari litoke nje ya wilaya na kufika eneo la tukio limechelewa kwa sababu linatoka mbali, tunaomba tupatiwe gari, " walisema.

Joseph Kimario, Mkazi wa Sanya Juu, aliiomba Serikali kuwapatia gari hilo ili kunusuru maisha yao na mali zao kuteketea kwa moto.

Akitolea mfano wa moto uliotokea kwenye maduka ya eneo la Kanisa Katoliki Sanya Juu, alisema takribani matano yaliteketea kwa kukosa gari la kwenda kuzima moto.

"Bidhaa nyingi tungeokoa, hapa wamefika (Zimamoto) saa moja wakati moto ulianza saa 12:30 asubuhi," alisema Kimario

Baraka Mmari, Mkazi wa Kobkoko, alisema Juni 5 mwaka huu, wakati nyumba ya jirani yao inaungua kwa jitihada zao, waliokoa baadhi ya mali.

Mmari, alisema kama gari la zimamoto lingekuwapo, wangedhibiti janga hilo.

Mkazi wa Ngarenairobi West Kilimanjaro, Festo Asenga, alisema kwa muda mrefu wanaomba kupelekewa gari hilo.

Asenga, alisema majanga ya moto yamekuwa yakitokea mara kwa mara na kusababisha hasara kwa wananchi kutokana na nyumba na mali kuteketea.

Paul Marigwa, Ofisa wa Ofisi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoji wilayani hapa, alisema walipata taarifa moto umezuka SanyaJuu na kuteketeza maduka.


Marigwa, alisema walichelewa kuzima moto huo baada ya gari kuchelewa kufika eneo la tukio kutoka Moshi mjini.

Alisema thamani ya mali zilizoteketea na moto haijafahamika na kwamba mtu mmoja amelazwa hospitali kwa matibabu baada ya kujeruhiwa.

Diwani wa Viti Maalumu, Egina Nzao, aliwashukuru wananchi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimomoto na Uokoaji na pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo kwa ushirikiano na kuhakikisha wanadhibiti moto huo usiendelee kuleta madhara sehemu nyingine.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Christopher Timbuka, alithibisha kutokea moto huo na kusema chanzo chake hakijafahamika.

Timbuka, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuchukua tahadhari wanapotumia umeme kuhakikisha wanazima vifaa usiku.





# MUWASA kufumua mabomba chakavu

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MAMLAKA ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) mkoani Mara inatarajia kutumia Sh. bilioni 2.9 kuondoa mabomba chakavu ili kuepuka hasara kutokana na upotevu wa maji na kuboresha huduma kwa wateja wake.

Mpango huo umetangazwa na Mkurungenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Nicas Mugisha wakati akijibu maswali ya viongozi wa serikali kwenye kikao cha Ushauri Mkoa (RCC) wa Mara kilichofanyika mjini hapa.

"Tumefanya tathmini za kuondoa mtandao wote wa mabomba hayo chakavu na kupata hitaji la Sh.bilioni 2.9, tayari tumeipeleka bajeti hiyo Wizara ya Maji," alisema.

Aliyataja maeneo yanayokabiliwa na tatizo hilo la mabomba chakavu kuwa ni Musoma, Tarime na Mugumu.

Alisema baada ya kufanya uchunguzi kwenye maeneo hayo walibaini kuwa kuna kilometa 75 za mabomba chakavu.

Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, alipendekeza mamlaka hiyo kuweka mpango mkakati wa kuvuna maji ya mvua zinaponyesha na kuwaondolea adha wananchi ya kukosa huduma hiyo kipindi cha kiangazi ambacho kinakuwa na ukame.

"Tumejenga vyoo, ingekuwa ni agizo la Mkoa ifungwe mitambo maalumu ya kuvuna maji ya mvua hiki kipindi cha mvua inyeshe saa sita kule vijijini kwa kila jengo jipya yatumike hata kwenye vyoo, kumwagilia bustani," alipendekeza Waitara.

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Tulinumpoki Mwakalukwa, alisema miradi 37 yenye thamani ya Sh. bilioni 24 inatarajiwa kukamilika Machi mwakani na kuwafikishia wananchi huduma.

"Kwa sasa tumeanzisha programu ya uchimbaji wa visima 900, kwa Mkoa wa Mara tunachimba visima 40 kwa maana ya vitano vitano kila jimbo kwa majimbo nane," alisema Tulimpoki.

# Marufuku bodaboda, bajaji kushindana barabarani

**Na Waandishi Wetu**

KIKOSI cha Usalama Barabarani kimepiga marufuku madereva wa bodaboda na bajaji kufanya mashindano barabarani ili kudhibiti ongezeko la ajali, vifo na ulemavu kwao na abiria.

Amri hiyo imetolewa na Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani nchini, Michael Deleli kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na madereva hao na wa bajaji katika mikoa ya Kanda ya Ziwa (Shinyanga, Mara na Mwanza).

"Acheni kuendesha pikipiki na bajaji kwa kushindana mkiwa barabarani na mmebeba abiria, mnasababisha ajali zisizo za lazima, abiria kupoteza maisha na kupata ulemavu wa kudumu," alisema Deleli na kusisitiza kuwa: "Tutahakikisha hili tunalidhibiti ili lisiendelee kujitokeza na tutashirikiana na viongozi wenu."

Akizungumzia kuhusu waendesha bodaboda na bajaji wasiokuwa na leseni, aliwaagiza askari wa kikosi hicho kuwakamata kwa kuwa wanachangia kukithiri kwa ajali nchini.

Alifafanua kuwa ametoa agizo hilo kutokana na vijana wengi kila uchao nchini wanajiunga na biashara hiyo ya kusafirisha abiria kwa vyombo hivyo.

Alisema hali hiyo imesababisha ongezeko kubwa la vyombo hivyo mitaani maeneo ya mijini na vijijini.

Alisema kutokana na ongezeko hilo, jitihada za haraka zinahitajika kwa askari hao kukabiliana na ajali kwa kuwakamata madereva wasiokuwa na leseni na wanaokiuka sheria barabarani. Alisema ajali hizo zimekuwa zikiongezeka nchini kutokana na mwendokasi, ulevi na ukiukaji wa sheria barabarani.

Deleli, kikosi hicho kinaendesha operesheni nchi nzima kuhakikisha vyombo hivyo vinakidhi matakwa ya kisheria ya usalama barabarani.

Aliwataka madereva nchini kuhudhuria mafunzo ya udereva na kukata bima kwa ajili ya kufidia hasara za upotevu wa maisha yao na abiria na mali wanapopata ajali.

Aliwataka viongozi wa madereva wa bodaboda na bajaji wa vijiwe kuweka utaratibu wa kuvaa sare ili kujitofautisha na watu wasio waaminifu.

Deleli, alisema uchunguzi umebaini watu hao wamekuwa wakifanya matukio ya uhalifu ya kupora simu za wananchi na lawama kuwaangukia wao na wanapofuatilia wanakuta sio dereva.

Mkuu wa kikosi hicho wa Kanda hiyo, Fatma Mbunja, alisema kuanzia sasa wanafanya ukaguzi wa vyeti vya mafunzo ya udereva kubaini halali na feki ili kudhibiti ajali hizo.

Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Mkoa wa Shinyanga, Idsam Mapande, aliahidi kuwafichua baadhi yao wanaoendesha pikipiki kwa mashindano ili wakamatwe na wachukuliwe hatua.

Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Kahama, Joshua Mkubwa, aliliomba jeshi hilo kuwadhibiti waendesha guta kwa kusababisha bodaboda kupata ajali barabarani.

**Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA), Ambrose Wantaigwa (TARIME), Vitus Audax (MWANZA).**




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha (kushoto) akikata utepe kuzindua kituo cha huduma Jumuishi "one stop center" wilayani Kishapu kwa ajili ya kutoa huduma kwa wahanga wa vitendo vya ukatili, ambacho kimejengwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kwa ufadhili wa Serikali ya Finland, kulia ni Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Schreiner, uzinduzi huo umefanyika juzi: **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC ataka usiri matukio ya ukatili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha amewataka Watumishi wa Kituo cha Huduma Jumuishi Wilaya ya Kishapu mkoani hapa kutunza siri za waathirika wa matukio ya ukatili ili kulinda heshima katika jamii.

Macha, alitoa kauli hiyo juzi kwenye hafla ya uzinduzi wa kituo hicho kilichojengwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kwa ufadhili wa Serikali ya Finland.

Aliwataka wakazi wa Kishapu kutumia kituo hicho kutoa taarifa za matukio hayo ili wapate huduma na haki na kuifanya jamii kuishi salama.

Alikemea ukatili mpya ambao umekuwa ukifanywa na akina mama kwa kuweka watoto mbele ya tangi la mafuta kwenye bodaboda na kuhatarisha afya na maisha yao.

Mkuu huyo wa wilaya, aliwasihi wazazi ifikapo Januari mwakani kuwaandikisha watoto wao kuanza darasa la kwanza katika shule za msingi baada ya kufikisha umri kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande wa sekondari, aliwasisitiza kuhakikisha wale waliochaguliwa wanajiunga na kidato cha kwanza katika shule za serikali ili kuanza masomo.

Macha, aliwaonya wazazi wanaowaficha watoto wenye ulemavu majumbani na kuwanyima haki yao ya kielimu, watakamatwa katika msako unaofanywa nyumba kwa nyumba na kufikishwa mahakamani.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Dk. Godfrey Kisusi, alisema

kwa kipindi cha Machi hadi Desemba, mwaka huu yaliripotiwa matukio ya ukatili 192, yakiwamo ya kimwili, ngono, kisaikolojia na utelekezaji watoto.

Dk. Kisusi, alisema kituo hicho kimesaidia upatikanaji wa huduma stahiki kwa waathirika wa matukio hayo na kuwekewa usiri.

Aliwasihi wananchi kutoa taarifa mapema za matukio hayo ndani ya saa 72 ili waathirika wapate huduma haraka na watuhumiwa kukamatwa.

Hata hivyo, Dk. Kisusi, alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa nyumba salama kwa ajili ya kuhifadhi waathirika wa ukatili hasa wanaopewa mimba za utotoni kwani wakirudi kwa wazazi wao hurubuniwa na kuharibu ushahidi kwa kuwakana watuhumiwa.

Mkuu wa Ushirikiano wa Ubalozi wa Finland nchini, Juhana Lehtinen, alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika mapambano ya ukatili wa kijinsia.



Ukurasa 14

**AJALI ZA NDEGE ZILIVYOTIKISA, KUUA VIGOGO AFRIKA, M/KATI**



Ukurasa 12

**2024 unavyowapa wapinzani mawazo yasiyoisha uchaguzi serikali za mitaa**


# siasa

JUMATANO DESEMBA 18, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


## MNYUKANO MBOWE, LISSU

# Unavyoelekea kufikia ujio Tanzania, CHADEMA mpya

**Na Restuta James**

HABARI kuu kisiasa hivi sasa ni uchaguzi wa viongozi wakuu wa CHADEMA, safari inayoanza na minyukano hadi kufikia mchuano mkali.

Pamoja na kwamba wagombea watatu wamejitokeza, mchuano mkali ni kati ya Mwenyekiti Freeman Mbowe na Makamu Tundu Lissu.

Mwanachama Odero Charles, anayejitosa kugombea pia hapewi wala hatajwi kwenye mitandao ya kijamii inayokosoa uwezo wa Lissu na Mbowe.

Wiki iliyopita, Lissu anautangazia umma nia ya kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, ili kukiongoza chama hicho kikuu cha upinzani, kuendesha siasa katika mazingira ya sasa anayosema ni CCM kutotaka uchaguzi wa ushindani ndani ya sanduku la kura.

Anasema kitendo cha asilimia kubwa ya wagombea wa upinzani kuenguliwa kwenye chaguzi 2019, 2020 na sasa 2024, kinawanyima wananchi haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Wakati Lissu akieleza hayo, Mbowe hajaweka wazi iwapo atagombea, licha ya kwamba amekaririwa akisema chama hicho hakijamzuia yeyote kugombea na kuhoji wanaomtaka astaafu 'astaafu aende wapi?'

Pamoja na kimya cha Mbowe, Katiba ya CHADEMA ya 2006, inampa nafasi ya kugombea tena kiti hicho, alichokikalia kwa miaka 20 sasa.

Ni kwa sababu inaondoa ukomo wa uongozi, ambazo zinatajwa na Lissu kuwa ilikuwa ni kuweka kinga ya viongozi ili waweze kukijenga chama kwa uhakika, kwa kuwa wangeendelea kusalia madarakani kwa muda mrefu ikiwa watafanya vizuri.



Mtiania Tundu Lissu, akipongezwa na wanachama muda mfupi baada ya kueleza uamuzi wa kugombea uenyekiti. **PICHA: RESTUTA JAMES**

**UKOMO UONGOZI**

Hili ndilo linalomfanya Lissu awe na agenda ya kuifumua katiba ya CHADEMA mara atakapotwaa madaraka.

"Nilipokwenda kujenga chama Singida Mashariki hakukuwa na viongozi wala wanachama, wachache tuliokuwapo tuligawana madaraka kutokana na uchache," anasema.

Miaka 18 iliyopita, katika maeneo mengi, viongozi wa CHADEMA wamepatikana mezani bila uchaguzi, kwa wanachama wachache wa eneo husika kupeana vyeo kuanzia mwenyekiti hadi mjumbe wa mwisho, anaongeza.

"Busara ya mwaka 2006 ilitulazimu tuondoe ukomo ili chama kisikose wanachama. CHADEMA imekuwa sana, hakuna nafasi inayotolewa kwenye 'kisahani' kama miaka 18 iliyopita," anafafanua Lissu.

Hata hivyo, anasema kwa mazingira ya sasa, kuweka vipindi vya kutumikia visivyo na mwisho, kunatengeneza watu kung'ang'ania madaraka na uchawa usio na sababu.

Anasema akichaguliwa kuwa mwenyekiti, atashirikiana na wenzake kuisuka katiba kwa nia ya kuweka ukomo wa madaraka pamoja na ubunge na udiwani wa viti maalum.

Anasema lengo ni kuruhusu mawazo mapya kuingia kwenye uongozi na wanawake wengi zaidi kwenye ubunge na udiwani.

Anasema nia yake ni kuwajengea wanachama wengi zaidi uzoefu wa uongozi na utumishi wa chama.

Lissu ambaye ni wakili kitaaluma, anasema nia nyingine ya kuisuka katiba ya CHADEMA kutengeneza mifumo bora ya uchaguzi ndani ya chama, ili ziwe huru na za haki.

Anaelezea pia kuwa kuna lengo la kuwa na tume huru kwenye chaguzi za chama, itakayoundwa na watu wasio na upande miongoni mwa wagombea.

Anasema kwa miaka 20 amekuwa kwenye Kamati Kuu ya CHADEMA, na kwamba ikitokea akashindwa kwa haki katika uchaguzi huo, atabakia kuwa mwanamageuzi.

"Kipindi cha siasa ngumu kinahitaji watu wagumu. Wanaoweza kusimama hadharani wakasema maneno yanayostahili. Wenye msimamo wa kuaminika. Wenye uadilifu usiokuwa na shaka. Huu ni muda sahihi kwangu kugombea nafasi hii ya mwenyekiti," anasema.

"Miaka 20 imenipa fursa ya kufahamu wapi panavuja, panapohitaji marekebisho na maboresho."

Anasema hana timu na kwamba kile ambacho anaweza kumwambia mtu mmoja anakisema hadharani pia.

"Utimu si siasa zangu. Mimi nazungumza hadharani, ndicho nitakachokuambia tukiwa wawili. Naamini kuna watu ambao wanafikiria kama mimi. Kwamba kipindi hiki kinahitaji aina tofauti ya siasa.

**LISSU NI NANI**

Kama anavyoeleza mwenyewe kuwa ni mwanachama ambaye ametumika katika ngazi mbalimbali muhimu na zenye dhamana kubwa kwa zaidi ya miaka 20.

"Nilianza utumishi wangu wa chama kama Mkurugenzi wa Katiba, Sheria na Haki za Binadamu, baadaye nikawa Mwanasheria Mkuu wa Chama. Kwa kipindi kifupi, nimewahi kuwa Mwenyekiti wa Kanda ya Kati; na tangu Desemba 2019, nimekuwa Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara," anasema.

Lissu amekuwa mbunge akiwawakilisha wananchi wa Singida Mashariki kwa vipindi viwili, hadi utumishi wake ndani ya bunge ulipokatishwa, akiwa kwenye matibabu.

Ni baada ya shambulio la risasi Septemba 07, 2017 kwenye nyumba za serikali jijini Dodoma.

Katika uchaguzi mkuu mwaka 2020, Lissu alipeperusha bendera ya CHADEMA kwenye nafasi ya urais, akichuana na John Magufuli wa CCM.

"Ninapenda kuamini kwamba, katika nafasi zote hizi, utumishi wangu kwa chama chetu na kwa nchi yetu, uliwapa ninyi wanachama na wananchi sababu kubwa ya kujivunia.

Nje ya utumishi wa chama chetu, kama mnavyokumbuka, nimewahi kushikilia nafasi ya Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), kufuatia uchaguzi wa kihistoria wa Machi 2017, katika kilele cha utawala wa kidikteta wa Rais John Pombe

INAENDELEA UK. 12



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na mabalozi wanaowakilisha nchi zao. **PICHA: IKULU**

# uchaguzi serikali za mitaa 2024 ulivyoibua maswali kwa upinzani

**NA MWANDISHI WETU**

MWAKA 2024 unaelekea ukingoni ukibakiza wiki mbili za kuuhitimisha ifikapo Jumatano Desemba 31 saa sita usiku. Unapomalizika, unakumbukwa kwa matukio mbalimbali yaliyojiri kwenye kipindi chote cha siku 365 na robo ambayo ni sifa ya mwaka mrefu.

Tukio muhimu kwa mwaka huu linalojiri kwenye siasa ni uchaguzi wa serikali za mitaa unaofanyika Novemba 27 na kusababisha gumzo kwa vyama vya upinzani baada ya CCM kuviacha mbali ikizoa viti vingi.

Itakumbukwa malalamiko ya vyama vya upinzani yanaanzia kwenye mchakato wa kuandikisha wapigakura kwenye daftari la mkazi, ukuchukuaji na urejeshaji wa fomu na hata wakati wa uchaguzi yakaibuka malalamiko likiwamo sakata la baadhi ya mawakala kuzuiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura.

Inadaiwa na upinzani kuwa baadhi ya wagombea wao walinyimwa fomu, huku waliobahatika kuzipata, wakishindwa kuzirejesha baada ya kuzijaza kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni watendaji kufunga ofisi.

|Lakini baadhi ya waliobahatika kurejesha fomu hizo, wakawekewa mapingamizi yakiwamo ya kukosea umri wao wengine wakidaiwa kuandika wana miaka 400 badala ya 40 na majina mfano Salim kusomeka Salama wakati jinsi ni mwanaume, hivyo kujikuta wakiwa nje ya ulingo huku wachache wakibahatika kupenya.

Hicho walichokiita 'figisu' kilisababisha CCM kupata ushindi wa wenyeviti wa serikali za vijiji kwa nafasi ya viti 12,150 sawa na asilimia 99.01. Waziri wa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa ndiye aliyatangaza matokeo hayo.

Matokeo hayo yaliyoacha vidonda vyenye maumivi kwa upinzani, Mchengerwa akitangaza matokeo anasema CHADEMA ilipata viti 97 sawa na asilimia 0.79 na kwamba vitongoji nane wagombea wake walifariki dunia.

Anataja maeneo ambayo wagombea walifariki baada ya uteuzi kuwa ni halmashauri za wilaya za Kilwa (2), Nanyumbu (1), Itilima (1), Ikungi (1), Manyoni (1), Uyui (1) na Mbarali na kwamba uchaguzi utafanyika tena.

Chama cha ACT-Wazalendo, kilipata viti 11, wakati CUF imebeba jumla ya viti 10, NCCR Mageuzi kiti kimoja.

Katika nafasi za mwenyekiti wa kitongoji anasema CCM ilishinda nafasi 62,728, CHADEMA nafasi 853 huku ACT-Wazalendo ikishinda nafasi 150, CUF nafasi 78, NCCR -Mageuzi imeshinda nafasi 10.

Aidha, anasema UDP ilishinda nafasi sita, UMD nafasi mbili na ADC nafasi moja.

Mwenyekiti wa mtaa, Waziri anasema CCM ilishinda viti 4213 sawa na asilimia 98.83 huku CHADEMA ikishinda nafasi 36 sawa na asilimia 0.84, ACT Wazalendo nafasi tisa sawa na asilimia 0.21, CUF nafasi 4 sawa na asilimia 0.09 na CHAUMA nafasi moja sawa na asilimia 0.02.

### OMBI LA CCM

Wiki chache kabla ya uchaguzi huo, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi kwa niaba ya chama chake anatoa wito kwa Wizara ya TAMISEMI kupuuza makosa madogo madogo katika hatua ya mwisho ya kusikiliza rufaa za mapingamizi.

Katibu Mkuu huyo anatoa ombi hilo kwa lengo la kuwapa Watanzania wengi zaidi nafasi ya kugombea kwenye uchaguzi huo ili kutoa hamasa ya demokrasia kuendelea kukua nchini.

"Natoa wito wa CCM kwa waziri mwenye dhamana na serikali za mitaa, kwamba tunatambua wamefuata sheria, lakini ni muhimu kukumbuka kwamba demokrasia yetu bado ni changa inahitaji kukua, tutachukua muda kujifunza makosa yataendelea kupungua, tunaomba TAMISEMI katika hatua ya mwisho ya rufani kuyapuuza makosa madogomadogo ili Watanzania wengi zaidi wapate nafasi ya kugombea. Msimamo wa CCM ni huu na nasisitiza msimamo huu ninaoutoa una baraka za Mwenyekiti wa CCM, Samia Suluhu Hassan".

Kauli hiyo ya Dk. Nchimbi inatokana na malalamiko ya vyama vya upinzani vikiwamo CHADEMA, ACT na CUF kulalamikia majina ya wagombea wao kuenguliwa kwa sababu mbalimbali.

Baadaye Waziri wa TAMISEMI Mchengerwa anaagiza wenye malalamiko kupeleka mapingamizi ambapo yaliwasilishwa kwa hatua ya kusikilizwa rufani za wagombea walioenguliwa.

Hata hivyo, uchaguzi ulimalizika kwa kilio ambacho na sasa vyama vikuu vya upinzani kikiwamo cha ACT-Wazalendo kimetangaza kutoutambua uchaguzi huo.

### MATAMANIO YA RAIS

Mwanzoni mwa mwaka huu katika sherehe za kuukaribisha mwaka huu ziitwazo (Diplomatic Sherry Party), Rais Samia Suluhu Hassan, anaahidi kuwa haki, demokrasia, sheria na utawala bora vitadumishwa wakati wote wa uchaguzi wa serikali za mitaa.

Anasema hayo kwa mabalozi wanaliopo Tanzania wanaoziwakilisha nchi zao pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, kwamba ili kuwa na uchaguzi huru na haki, kikosi kazi huru cha kupitia na kushauri mageuzi muhimu katika mfumo wa siasa kiliundwa na kiliwasilisha ripoti yake mwaka 2023.

Kwa mujibu wa Rais, mapendekezo mengi ya kikosi kazi yaliyopokelewa na serikali na wadau wote, yalihusu kuongeza uwazi katika mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na uteuzi wa mwenyekiti wa tume ya uchaguzi.

Lakini anasema masuala machache hayakupokelewa moja kwa moja ambayo yalikuwa kinyume na katiba, na kwamba yanaweza kuchukuliwa wakati wa mchakato wa katiba.

Anasema serikali itaendeleza ushirikiano na balozi hizo kwa mujibu wa katiba, tunu za taifa, usawa, umoja na mshikamano wa kitaifa, lakini akawataka mabalozi hao kutoingilia uchaguzi na kuzingatia mila, kanuni na maadili ya kidiplomasia.

# UNAVYOELEKEA KUFIKIA UJIO TANZANIA, CHADEMA MPYA

**INATOKA UK. 11**

Magufuli," anasema.

Anasema tangu akiwa kijana, amekuwa mwanaharakati na mwanasheria jasiri katika masuala ya ulinzi wa mazingira na utetezi wa haki za binadamu.

Wakili, Lissu ni mmoja wa mawakili wa Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT), aidha amewahi kuwa mtafiti katika masuala ya rasilimali za asilia katika Taasisi ya Rasilimali za Dunia (WRI), yenye makao makuu yake Washington DC nchini Marekani.

"Ninaamini kwamba wanachama wenzangu mnaamini, kuwa nina sifa za kutosha za kugombea nafasi ya juu kabisa ya uongozi katika chama chetu ya Mwenyekiti wa Chama Taifa, kama zilivyoainishwa katika ibara ya 10.2 ya katiba," anasema.

Uamuzi huo unafuta barua yake ya Agosti 06, 2024 aliyoiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, kutia nia ya kugombea nafasi anayoishikilia sasa, yaani Makamu Mwenyekiti.

Uamuzi wa Lissu umeibua maswali kwa baadhi ya makada wa chama hicho, ambao wanahoji sababu za kufuta barua yake ndani ya muda mfupi, wengine wakisema anagombea kwa shinikizo kutoka kwa watu wasioitakia mema CHADEMA.

Wanamtaja Lissu kuwa ataiweka CHADEMA kwenye hali ya sintofahamu kutokana na misimamo yake, hasa kutopenda mazungumzo na upande usioamini kile anachokiamini.

### MWENYEKITI MBOWE

Wanaomuunga mkono Mbowe, wanamwona kama kiongozi aliyechangia kukua kwa CHADEMA kwa kuwa na mikakati na timu iliyokiwezesha kutwaa mitaa, vijiji na vitongoji vingi mwaka 2014 na wabunge na madiwani wengi kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2015.

Wanaona kwamba ni katika uongozi wa Mbowe, CHADEMA imekua na wanachama wengi, amejenga imani kubwa kwa umma kwamba ni makini kinachoweza kuongoza kambi rasmi ya upinzani bungeni, halmashauri, manispaa na majiji makubwa, likiwamo Dar es Salaam.

"Mbowe ni mwanadiplomasia, anajua siasa na kubwa zaidi ni mtu aliyeibua wanasiasa wengi vijana akawajenga na kuwatangaza kwa umma kiasi cha wengine kudhihirika kuwa wanafaa na leo wanahudumu serikalini," anasema Julius Massawe, kada wa CHADEMA mkoani Kilimanjaro. Wengine wanasema diplomasia ya Mbowe imefanikisha kuwavuta mawaziri wakuu Edward Lowassa na Frederick Sumaye, kujiunga na CHADEMA, uamuzi wanaoona pengine hauwezi kufanywa na Lissu.

WANAWAKE WASEMA

# Dira wanayoitaka ni ile inayokuza uchumi na kuondoa umaskini

**NA MWANDISHI WETU**

MAHITAJI ya kuwa na uchumi unaogusa na kuondoa umaskini, kuainisha gharama na hasara zitokanazo na ukatili wa kijinsia (GBV) kwa taifa na kujenga viwanda vinavyomilikiwa na wanawake, ni mambo yanayotajwa na kinamama kuwa lazima yaingie kwenye dira ya maendeleo ya taifa ya 2050.

Ni maoni ya Mtandao wa Wanawake na Dira, kwa wajumbe wa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, wanapokutana kuhakiki rasimu ya dira.

Akifungua pazia la mjadala, Profesa Ruth Meena anasema licha ya rasimu wa dira kutaja kuwa uchumi umekua kwa kipindi cha 2020 hadi 2025, hakuna uhalisia kwasababu haukugusa umaskini.

"Uchumi ulikua lakini umaskini unaongezeka, huko ni kukua kwa vitu lakini sio watu, hata Mwalimu Julius Nyerere alisema uchumi hauwezi kukua kama hauondoi umaskini." Anakumbusha. Anawaambia wajumbe wanaokutana na wadau kuhakiki rasimu ya dira ya taifa kuwa lazima dira ionyeshe kuwa taifa linahitaji kuwa na uchumi imara, jumuishi na linganifu unaogusa wanawake na wanaume.

Aidha, hakuna maendeleo kiuchumi kama vikwazo vya kibiashara na uzalishaji vinavyowabana wanawake na kuwabakiza kwenye sekta isiyo rasmi havitaondolewa na dira inayoandaliwa. Anasema wanawake wanachuuza mboga, matunda kwenye mabeseni mijini, ni mamalishe pembeni ya barabara wakiuza vyakula mbalimbali.

"Lazima kuondoa vikwazo na kuwawezesha wainuke na kufanya biashara kubwa, wamiliki kampuni na viwanda, si uchuuzi na hilo dira ilianishe," Profesa Ruth anasema.



Mwanamtandao wa wanawake na dira, Rose Marando, akichangia maoni kuboresha rasimu ya dira walipokutana wajumbe wa Tume ya Mipango na Naibu Waziri Stanslaus Nyongo (kuliai). **PICHA: MWANDISHI WETU**

### HASARA GBV

Profesa Ruth anasema ukatili wa kijinsia unaligharimu taifa kwenye nguvukazi, tiba, afya ya akili na hata vifo. Kwa hiyo lazima utafiti ufanyike ili kujua hasara na madhara yake kwa nchi.

Anafafanua kuwa wanawake wakiumizwa hawazalishi, wala kutunza na kuhudumia familia, wanahitaji tiba, wanapata matatizo ya shida ya akili, hivyo kurudi tena kwenye umaskini.

"Tunataka utafiti wa hasara GBV ufanyike na takwimu zinazotolewa na mashirika mbalimbali ya kijamii kuhusu wanawake, zitumike ili kupata uhalisi wa madhara, hasara na athari kwa nchi," anasema.

"Tunapotambua madhara yake, tunafahamu hasara kiuchumi, gharama kwenye afya, malezi kupoteza nguvu kazi, mapato ya mwanamke na taifa."

### VIWANDA VIDOGO

Wana mtandao wanataka dira ianishe inapozungumzia uchumi wa viwanda, ni viwanda gani itamke kuwa ni viwanda vidogo na vikubwa vinavyomilikiwa na wananchi.

"Tunahitaji viwanda vidogo vinavyomilikiwa na wanawake vijijini na popote penye uhitaji. Kwa mfano matunda yanaoza barabarani, wanawake wanasuka mikeka vikapu, nyungo na mapambo wako barabarani hakuna soko.

Kwa nini tusijenge viwanda vidogo wakavilimiki? Wakaongeza mnyororo wa thamani wakakua kiuchumi na kuondoa umaskini?" anasisitiza.

Anasema ni wakati dira ya 2050 kuainisha ulazima wa wanawake kupewa ujuzi wa kuzalisha, kufungasha na kuuza bidhaa kutoka kwenye kampuni na viwanda vidogo wanavyomiliki iwe vijijini na popote kwenye unafuu wa upatikanaji wa malighafi.

### AMANI/USALAMA

Rebecca Gyumi anazungumzia msingi mkuu wa dira wa utawala bora, amani, usalama, utulivu na umoja akisema rasimu ya dira inachukulia uwepo wa amani kwa mtazamo wa 'kizamani' unaomaanisha ni ukosefu wa vita, wakati si hivyo tu.

"Amani ni zaidi ya kukosekana vita, ni kitu kinachoanzia nyumbani, kwa hapa kwetu GBV inakosesha watu wengi amani, wanawake, watoto na wale wanaotuhumiwa kwa uhalifu wanachomwa, albino wanauawa, watoto wananajisiwa ni ukosefu wa amani," anasema Rebeca.

Anataka dira ifafanue kuhusu amani kuwa ni usalama wa kila mtu, iwe nyumbani, sehemu za kazi, ndani ya jamii, shuleni na taifa zima.

Rebeca anakumbusha kuwa iwapo msingi mkuu wa dira ni utawala bora, usalama, amani na utulivu, lakini wanawake wengi, wazee, watoto, wenye mahitaji maalum (albino), wanakatiliwa, hawako salama na kwamba ni vigumu kuwa na taifa na raia wenye kujivunia uwepo wa amani na usalama.

### TEHAMA

Anazungumzia usalama na amani kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na mifumo ya kidijitali kuwa inahatarisha amani, akitolea mfano kuwa inatumika kufanya mashambulizi ya kimtandao dhidi ya wanawake, watoto hata taifa.

"Kwa hiyo dira ionyeshe namna ya kujilinda dhidi ya mashambulizi ya kimtandao kwa watu na taifa. Nchi inaweza kuanzisha vita vya kimtandao dhidi ya nchi nyingine na kuvuruga uchumi na maendeleo ya kijamii," anaonya.

### BIMA YA AFYA

Akiwasilisha umuhimu wa bima ya afya kwa kila Mtanzania, Janeth Mawinza, anataka dira itamke kuwa tiba ni haki ya kila Mtanzania bila kujali kipato, hadhi wala makazi.

"Bima ya afya ni kama imebagua imewaacha nje wanawake, ambao wengi hawana ajira, ndio mama lishe, wauza mboga, wachuuzi wa biashara ndogo. Hao ndio wanaowatunza watoto kulea na kutunza familia, lakini hawana bima ya afya," anasema Janeth.

Anasema wanapoumwa, wanaacha uzalishaji watafute dawa kwa ajili ya gharama za kujitibu na kutibu watoto, wakati mwingine hawana pesa za kutosha wanapata huduma duni na hii inachangia vifo vya watoto, kinamama na wanafamilia wengine.

"Ndio maana tunasema bima ya afya iwe ni kwa kila Mtanzania bila kujali kingine chochote kwa sababu utaratibu uliopo hauwagusi wote," anasema.

### ELIMU USALAMA

Dk. Avemaria Semakafu anazungumzia kipengele cha kuwana jamii iliyoelimika inayomudu ushindani ndani ya dira akisema pengo linalotakiwa kuzibwa ni dira izungumzie uwepo amani na usalama shuleni.

Ianzie shule ya msingi, sekondari, vyuo vya kati na vikuu iwe ni sehemu salama ya kusoma kwa wote, wenye ulemavu na wazima, kusiwe na GBV.

Anakumbusha ukosefu wa usalama shuleni umesababisha wanafunzi kukwama kielimu na kuongeza kuwa taifa linapoingia kwenye uchumi wa kati, raia walioelimika ni kigezo muhimu cha kufikia lengo hilo.

Akijibu hoja za wana mtandao wanawake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo, anawapongeza wana mtandao hao kwa maoni yanayosimama imara kutetea wanawake wote wa Tanzania.

Anasema wanawake wamewasilisha maoni ambayo yanazingatiwa, kwa kuwa hata sasa tume inaendelea kupokea maoni na ushauri kutoka kwa watu mbalimbali.

"Niseme mmewasilisha maoni yenye tija yanayosimamia haki za wanawake wote wa Tanzania. Niseme mmeupiga mwingi," anasema Nyongo.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ajali za ndege zilivyotikisa, kuua vigogo Afrika, M/Kati




Mkuu wa Majeshi wa Kenya, Francis Ogolla na Ebrahim Raisi wa Iran (picha chini) walipoteza maisha kwenye ajali za ndege 2024: **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI 2024 ukibakiza wiki chache kumalizika, yako matukio ambayo yameacha kumbukumbu kwenye uwanja wa kimataifa kama vile ajali na vita.

Ajali za ndege zimeua viongozi Afrika pamoja na Mashariki ya Kati mataifa ya Palestina na Iran.

Juni mwaka huu, inasikika ajali ya ndege, ikimaliza maisha ya aliyekuwa Makamu wa Rais wa Malawi, Dk. Saulos Chilima.

Ajali hiyo ilisababisha kifo chake na abiria wengine huku ikiacha simanzi kwa familia, wafuasi na Wamalawi.

Chilima na maofisa wengine alikuwa akisafiri kuhudhuria mazishi ya aliyekuwa waziri wa serikali hiyo, Ralph Kasambara.

Mke wa rais wa zamani Bakili Muluzi, Shanil Dzimbiri ni miongoni mwa abiria waliokuwa kwenye ndege hiyo.

Ndege aina ya Dornier 228 ilitangazwa kupotea kwenye rada ilipofikia eneo la hifadhi ya misitu Chikangawa na Juni 11, mwaka huu, ikathibitishwa imepata ajali.

Chilima, alikuwa mwanasiasa maarufu katika siasa za Malawi, na kabla ya kujiunga na siasa alichangia kukua kwa kampuni ya Airtel nchini humo na kukuza mapato.

Kisiasa, alihudumu katika kiti hicho tangu mwaka 2014 akipambana na rushwa na kukumbana na changamoto kadhaa. Mazishi ya kitaifa yaliangaza mchango wake katika nchi.

Chilima alikuwa amerejea muda mfupi kutoka katika ziara ya kikazi nchini Korea Kusini, kwenye kongamano la Korea Afrika Summit, jijini Seoul.

Kabla ya kifo cha Chilima, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini Kenya, Francis Ogolla, anaangamia kwenye ajali ya ndege, Mei mwaka huu.

Ulikuwa mwaka wa ajali za anga ambayo pia ilikatisha uhai wa Rais wa Iran, Ebrahim Raisi, yote yakiacha simanzi kwa mataifa wafiwa.

### KILIO KENYA

Aprili, mwaka huu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini Kenya, Francis Ogolla alifariki kwa ajali ya helikopta.

Rais wa Kenya, William Ruto anatangaza kifo cha Ogolla pamoja na maofisa wengine tisa wa jeshi, huku wawili wakinusurika.

Ogolla anafariki baada ya helikopta aliyokuwa akisafiria pamoja na maofisa wengine kuanguka eneo la Kaben, Marakwet.

Ogolla alichukua nafasi ya kuongoza jeshi tangu Aprili 28, mwaka 2023.

Mashuhuda wanasema ndege ilishika moto wakati wa kuanguka. Eneo hilo lilizingirwa baada ya ajali hiyo.

Maofisa hao walikuwa wakichunguza eneo hilo, kabla ya kutumwa kwa wanajeshi zaidi kukabiliana na wezi wa mifugo.

Helikopta hiyo ya Jeshi la Anga la Kenya aina ya Huey, ilikuwa imetoka katika shule moja ya msingi kabla ya kuanguka na kuwaka moto.

Ogolla, alichukua uongozi wa jeshi kutoka kwa Jenerali Robert Kibochi, baada ya kufikisha umri wa kustaafu.

### SIMANZI IRANI

Mei, mwaka huu, Rais wa Iran, Ebrahim Raisi, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Hossein Amir-Abdollahian na wengine saba, walifariki dunia katika ajali ya helikopta iliyotokea kaskazini-magharibi mwa Iran.



Shirika la Habari la Serikali (IRNAA), linasema ndani ya ndege hiyo pia alikuwamo Ayatollah Mohammad Ali Al-e Hashem, imamu wa Swala ya Ijumaa katika mji wa Tabriz na Jenerali Malek Rahmati, Gavana wa Jimbo la Iran la Azabajani Mashariki.

Kamanda wa Kitengo cha Ulinzi wa Rais, Sardar Seyed Mehdi Mousavi, pia aliuawa, pamoja na walinzi kadhaa na wafanyakazi wa helikopta ambao bado hawaja tajwa.

### MAUAJI HAMAS

Wanajeshi wa Israel walikuwa wanamwinda kwa zaidi ya mwaka mmoja kiongozi wa Hamas, ambaye alitoweka huko Gaza mara tu baada ya kupanga mashambulizi ya Oktoba 7, mwaka 2023.

Yahya Sinwar (61), inasemekana alitumia muda wake mwingi kujificha kwenye vichuguu chini ya ukanda huo, pamoja na kada ya walinzi na ya mateka waliokamatwa kutoka Israel.

Jeshi la Ulinzi la Israel, linasema kuwa kikosi cha 828 cha Biislamach Brigade kilikuwa kikishika doria Tal al-Sultan, eneo la Rafah.

Lakini hatimaye, alikutana na mwisho wake katika kukutana na doria ya Israel kusini mwa Gaza, alikuwa na idadi ndogo ya walinzi. Hakuna mateka walioptikana.

Wanamgambo watatu walitambuliwa na walipambana na wanajeshi wa Israel na wote waliuawa.

Kifo cha Sinwar ni pigo kubwa kwa Hamas, lakini haukuwa mwisho wa vita.

Mwili ulitolewa na kupelekwa Israel, baadaye eneo hilo liliwekwa salama.

Daniel Hagari, msemaji wa IDF, alisema vikosi vyake "havikujua kuwa alikuwa huko lakini tuliendelea kufanya kazi, alikimbia peke yake kwenye moja ya majengo na aliuawa baada ya kupatwa na ndege isiyo na rubani."

### MILIPUKO YA SIMU

Tukio lingine kwa mwaka huu, ni vifo vya takribani watu 26 wakiwamo watoto wawili, waliuawa na maelfu ya wengine kujeruhiwa.

Wengi wao wakiwa vibaya, baada ya vifaa vya mawasiliano vingine vinavyotumiwa na kundi lenye silaha la Hezbollah, kulipuka kwa kiasi kikubwa kote nchini Lebanon.

Katika tukio la milipuko, ilijeruhi takribani watu 450, kulingana na Wizara ya Afya ya Lebanon.

Milipuko hiyo ilitokea karibu na umati mkubwa wa watu waliokuwa wamekusanyika, kwa ajili ya mazishi ya wahanga wanne wa milipuko hiyo ya Jumanne.

Milipuko hiyo ilizidisha hali ya wasiwasi katika jamii ya Lebanon, ikitokea siku moja baada ya shambulio kama hilo.

Makampuni mawili yaliyoko Taiwan na Hungary yanayoshutumiwa katika ripoti za vyombo vya habari kwa kutengeneza vifaa hivyo na nchi zote hizo zilikana kuhusika.

### KUONDOSHWA ASSAD

Rais wa Syria, hivi karibuni na serikali yake ameng'olewa madarakani. Bashar al-Assad, alitolewa kimabavu baada ya kundi la waasi kuongoza maasi dhidi yao Jumapili, Desemba 8, 2024.

Familia ya Assad imeitawala Syria kwa miaka 53, Assad alichukua madaraka mwaka 2000, baada ya babake kutawala kwa miaka 30.

Miaka 13 iliyopita, anatumia nguvu kuwakandamiza waandamanaji na kisha kukawa na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Zaidi ya watu 500,000 wameuawa na wengine milioni 12 wamelazimika kukimbia makazi yao.

Lakini Jumatano wiki iliyopita, kundi la Kiislamu, Hayat Tahrir al-Sham (HTS), lilifanikiwa kufanya mashambulizi mabaya kaskazini magharibi mwa nchi hiyo, baada ya kushirikiana na makundi mengine ya waasi.

Waasi hao waliuteka mji wa pili kwa ukubwa nchini Syria, Aleppo na kuelekea kusini hadi mji mkuu, Damascus, ambako walizidi nguvu jeshi la Syria.

Russia, baadaye ilitangaza kuwa Assad na familia yake wamepewa hifadhi ya kisiasa huko Moscow.

### MOTO GAZA

Tangu kuanza kwa vita huko Ukanda wa Gaza, idadi ya vifo imefikia watu 45,000 kwa mujibu wa kituo cha Aljazeera.

Sasa vita hiyo inatimu miezi 15 ni kati ya matukio ya kimataifa ambayo yamekuwa yakiwaumiza vichwa wapatanishi wa kimataifa.

Katika idadi hiyo ya vifo wamo watoto 17,000 achilia mbali watu 11,000 ambao wameripotiwa kutoweka wakihofiwa wamefukiwa na vifusi.

***BBC***





# Machali ahamasisha wakulima wajisajili

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WAKULIMA wilayani hapa Mkoa wa Singida wametakiwa kujisajili katika mfumo ili wapatiwe mbegu na mbolea za ruzuku kutoka serikalini.

Wito huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Mosses Machali, wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Ilunda Kata ya Ilunda katika hafla ya kumkabidhi zawadi mshindi wa tuzo ya mkulima bora kitaifa wa maonesho ya kilimo na mifugo maarufu Nanenane kwa mwaka huu.

"Serikali ilianza na mbolea na sasa imeanza kutoa ruzuku kwenye mbegu za mahindi na alizeti, wito wangu kwenu nendeni mkajisajili ili muweze kupata mbegu kwa bei nafuu," alisema.

Kuhusu utunzaji wa mazingira, Machali aliwataka wakazi hao kupanda miti ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kutokana na kuwa janga duniani.

"Niwaombe mjitahidi kupanda miti, tukiwa na miti mingi tutapata mvua za kutosha na tutakuwa tumetunza mazingira na kuendesha kilimo chetu vizuri kwa sababu mvua zitakuwapo za kutosha," alisema.

Machali aliwakumbusha wakazi wa wilaya hiyo kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani, kufanya kazi kwa bidii na kujilinda dhidi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alitoa wiki mbili kwa wakuu wa Idara ya Kilimo mkoani humo kuhakikisha wanawasajili wakulima hadi kufikia asilimia 85 kwa ajili ya kupata pembejeo za kilimo, la sivyo waandike barua kuacha kazi.

"Acheni uvivu na kuniletea maneno ya uwongo mimi sitawaacha nataka kuona hadi kufika mwisho wa msimu wa kilimo nani ananikwamisha," alisema.

Dendego alisema suala la kilimo kwa Singida ni linatakiwa kupewa kipaumbele namba moja, hivyo hatakubali kuona baadhi ya maofisa ugani wanakwamisha jitihada za serikali katika kuinua sekta ya kilimo mkoani humo.

**"Serikali ilianza na mbolea na sasa imeanza kutoa ruzuku kwenye mbegu za mahindi na alizeti, wito wangu kwenu nendeni mkajisajili ili muweze kupata mbegu kwa bei nafuu," alisema.**

# Wahamasishwa kuchangamkia Hatifungani za Rais Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ya Mkoa wa Dodoma imetoa wito kwa wananchi kuchangamkia ununuzi wa Hatifungani za Samia ili kuharakisha maendeleo.

Rai hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, wakati hatifungani za Sh. bilioni 1.5 zikiwa zimenunuliwa na baadhi ya wafanyabiashara, wakandarasi na viongozi kwa mikoa ya Kanda ya Kati.

Senyamule alitoa rai hiyo jana kwenye uzinduzi wa ununuzi wa hatifungani hizo kwa kanda hiyo iliyoratibiwa na Benki ya CRDB kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

"Hatifungani hizi ni muhimu sana kama mkoa tunahitaji miundombinu mingi ya kuendeleza sekta ya barabara, hivyo tujitokeze kununua kwanza kwa ajili ya kupata faida yetu wenyewe na pili ni kuharakisha maendeleo ya mkoa wetu," alisema Rosemary.

Alifafanua kuwa mapato yatakayopatikana kwenye hatifungani yatasaidia kutekeleza miradi ya barabara inayoendelea na mipya nchini na kanda hiyo.

"Ni utashi mkubwa wa Rais Samia Suluhu Hassan kufanya maendeleo kwa ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi, kama serikali tuna kasi tunayokwenda nayo kulingana na uchumi wetu," alisema na kuongeza kuwa:

"Kuna watu wengine wana fedha wanaweza kujiwekea akiba zao kwenye hatifungani na zikatumika kuharakisha kujenga miundombinu yetu."

Alisema kuweka kwenye hatifungani ni salama na benki hiyo itasaidia kutengeneza faida na kuchochea kuleta maendeleo ya haraka ya taifa.

"Hatifungani hii ni ya kwanza kutolewa nchini na lengo ni kuwaunganisha wananchi wa vijijini na mijini kwa maendeleo na kuchochea ustawi wa taifa kwa kuwa sekta binafsi na serikali zinaungana kujenga nchi kwenye maendeleo," alisisitiza mkuu huyo wa mkoa.

Naibu Katibu Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Rogatus Mativila, alisema lengo la hatifungani hizo ni kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA.

Mativila, alisema hatifungani hiyo imechambuliwa na wataalamu na kukubaliana ianzishwe ili kuchochea ujenzi wa miundombinu.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima ambaye anakaimu Mkoa wa Iringa, alisema nchini India wamefanikiwa kwenye miundombinu kupitia hatifungani na kumshukuru Rais Samia kwa wazo hilo zuri na kama litachochea ujenzi wa miundombinu nchini.

"Tunakwenda kuhamasishana ngazi za halmashauri pia ili wananchi waone manufaa ya Samia Infrastructure Bond, ili kila halmashauri iwekeze kwenye mapato yake na itasaidia kupata fedha za kujenga miundombinu," alisema Malima.



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Moses Machali, akizungumza jana na wananchi wa kijiji cha Ilunda, Kata ya Ilunda wilayani humo katika hafla ya kumkabidhi zawadi mshindi wa tuzo ya mkulima bora kitaifa wa maonesho ya Nanenane 2024. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Mgawo maji mbioni kwisha Dodoma

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imeanza kutekeleza mkakati wa kuchimba visima vya maji ili kutatua kero ya mgawo wa maji katika Jiji la Dodoma.

Naibu Waziri wa Maji, Mathew Kundo aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi ya maji inayotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Kundo, alisema serikali imeendelea na mikakati hiyo ya muda mfupi ili kusaidia kupunguza tatizo hilo kwa kuanza kuchimba visima vitano eneo la Nzunguni, Kisasa na Nala.

Alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 10.3 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Nzuguni na ujenzi wake umefikia asilimia 87.

Alisema mradi wa eneo la Nala utagharimu Sh. bilioni 3.3 kwa visima vyote viwili hadi sasa cha kwanza utekelezaji umefikia asilimia 98.

Alisema mpango wa muda wa kati ni kuvuta maji ya Bwawa la Farkwa kuyafikisha jijini Dodoma.

Naibu Waziri huyo, aliutaja mkakati wa muda mrefu kuwa ni kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria ambayo pia yatasambazwa kwa mikoa ya Tabora na Singida.

Aliwataka DUWASA kuanza kuvuna maji ya mvua ili kuongeza vyanzo vya maji na kukabiliana na ukosefu wa huduma hiyo kwa wateja.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Aron Joseph, alisema kwa sasa uhitaji wa maji katika jiji hilo ni lita milioni 149 kwa siku, ambazo ni nyingi ikilinganishwa na zinazozalishwa lita milioni 79.

Joseph, alisema miradi hiyo mitatu ikikamilika, itakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 90 kwa siku.

Alisema katika miradi hiyo, mamlaka imekuwa na utaratibu wa kuwawekea wananchi sehemu ya kupata huduma ya maji.

Akizungumzia kuhusu mipango ya baadaye mamlaka hiyo, alisema ni kusambaza vichoteo vingi ya maji kwenye maeneo vilipochimbwa visima hivyo.

Awali Katibu Tawala Wilaya ya Dodoma, Sakina Mbugi, alisema watahakikisha wanafuatilia kwa karibu miradi inayotekeleza kwa kushirikiana na wananchi.

Sakina, aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa serikali kwa kutoa maeneo yao inakotekelezwa miradi hiyo ili kuepuka kukwama.





# Gesi yateketeza mgawaha, maduka

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

BAADHI ya wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma wamekumbwa na taharuki baada ya mitungi mitatu ya gesi kufumuka na kushika moto kisha kuteketeza mgahawa wa Delight Garden na maduka

Akizungumza na waandishi wa habari Kaimu Kamanda wa Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ruvuma, Merania Nyabwinyo alisema kuwa tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki iliyopita asubuhi kwenye bustani ya halmashauri hiyo.

Nyambwinyo, alisema jeshi hilo lilipokea taarifa kwa njia ya simu kuhusiana na tukio hilo na kupeleka kikosi chake kuzima moto.

Alisema kikosi hicho kilifanikiwa kuzima moto huo licha ya kuwa baadhi ya bidhaa zilizokuwemo zilikuwa zimeungua.

Nyabwinyo, alisema kwenye eneo hilo kulikuwa na maduka ya chakula na vinywaji.

"Chanzo cha moto huu bado hakijafahamika, tunaendelea kuchunguza ili kubaini chanzo halisi, tunatoa wito kwa wananchi kutoa taarifa ya matukio mbalimbali mapema iwezekanavyo kwenye ofisi zetu na si vinginevyo," alisema Nyabwinyo.

Mkurugenzi wa mgahawa huo, Hamza Mohamed alisema huo moto ulianzia jikoni ambako kulikuwa na mitungi mikubwa mitatu ya gesi.

Mohamed, alisema inahofiwa mitungi hiyo ilipokea joto la mvuke kutoka kwenye sufuria la mboga ambalo lilikuwa limefunikwa na kulipuka.

"Baadaye ule mfuniko uliruka kutokana na msukumo wa mvuke na kuenea kwenye chumba hicho cha jiko kisha mitungi yote mitatu kulipuka moto," alisema.

Alisema katika tukio hilo vibanda 11 vilivyopo kwenye eneo hilo vimeteketea kwa moto na vingine 25 kunusurika baada ya kikosi hicho kufika na kuwahi kuzima.

Kwa mujibu wa mmliki huyo, hadi sasa thamani ya mali zilizoteketea kwa moto huo haijafahamika, wanaendelea kuchunguza.





Mkuu wa Wilaya ya Iringa Kheri James (wa tatu kushoto) akimkabidhi mmoja kati ya vijana 75 wa Mradi wa Feed The Future Tanzania ambao wamepatiwa vifaa vya kilimo na ufugaji vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuendesha shughuli zao kisasa. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# TRA kukusanya trilioni 3.4/- Desemba

**Na Mwandishi Wetu,**
Njombe

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) inatarajia kukusanya zaidi ya Sh trilioni 3.4 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa kipindi cha mwezi huu.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo aliyasema hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa na kuzungumza na wafanyabiashara katika maeneo yao ya biashara.

Kayombo, alisema mamlaka hiyo imepanga kukusanya kiwango hicho cha fedha ikiwa ni pamoja na kukusanya kodi kwa wafanyabiashara.

Alisema mamlaka hiyo itakusanya kiwango hicho kutokana na wafanyabiashara wengi kulipa kodi zao mwezi huo wa Desemba kukusanya mapato mengi kutokana na kuuza bidhaa nyingi msimu wa sikukuu za Krismas, mwaka mpya na mahitaji ya wanafunzi.

Akizungumza kuhusu ujio wake mkoani Njombe, Kayombo, alisema ni kwa ajili ya kuhimiza wafanyabiashara kulipa kodi ili kuhakikisha mamlaka hiyo inapata mapato ya kutosha.

"Kwa mwezi huu lengo ni trilioni 3.4 na ni lengo kubwa kuliko miezi mingine yote kwa hiyo hatuwezi kulifikia bila ya ushirikino, tuhamasishane ili tuweze kulitimiza," alisema Kayombo.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wafanyabiashara nchini kulipa kodi kwa hiari ili kuiwezesha serikali kutekeleza miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli zake.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema serikali itaendelea kuhimiza wafanyabiashara na wananchi kulipa kodi.

"Lengo ni kuwaleta pamoja wafanyabiashara na kuondoa manung'uniko kwa hiyo watu wanalipa kodi kwa hiyari yao, wanalipa kodi wakiwa na amani kwamba wanachangia kitu kwenye nchi yao," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Halmashauri ya Mji Njombe, Eliud Pangamawe, alisema wanasisitiza mahusiano mazuri na maofisa wa mamlaka hiyo na serikali na kuhamasisha wafanyabiasha waendelee kulipa kodi..

# Wahimizwa maandalizi wanafunzi kidato cha kwanza

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

WAZAZI na walezi wilayani hapa Mkoa wa Njombe, wametakiwa kufanya maandalizi mapema ya mahitaji ya wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza Januari 13, mwakani.

Wito huo ulitolewa juzi na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Njombe, Hitra Msola wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Lilombwi na Liwengi Kata ya Kifanya iliyopo Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Msola alisema ni wajibu wa wazazi na walezi kuhakikisha ifikapo Januari mwakani, wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shule bila ya vikwazo.

Aliwataka viongozi wa serikali za vijiji na mitaa kuhakikisha wazazi watakaoshindwa kuwapeleka watoto wao shule wanachukuliwa hatua.

Aliwataka wale wasio na uwezo, serikali za kijiji na mitaa kuona namna ya kuwasaidia watoto wao waende shule badala ya kuwaacha mtaani.

"Kule shuleni hakuna ada, tukajiandae kila kitu kitakwenda kwa sababu serikali imejenga madarasa na kazi yako mzazi ni kuandaa mazingira ya shuleni ili mtoto ale chakula ashibe, tukifika Januari tusikwepe tupeleke watoto shule," alisema Msola.

Katibu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM ya Wilaya hiyo, Singo Ndoera aliwakumbusha wazazi kutambua kuwa urithi pekee wa watoto ni elimu.

Katibu wa Mbunge wa Njombe Mjini, Andrea Mahali, aliwataka wakazi wa vijiji hivyo kuendelea kulinda maeneo yao dhidi ya uuzaji holela wa ardhi na uharibifu wa mazao ya misitu.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Liwengi, Costantino Mfugale, alisema watahakikisha watoto wanapelekwa shuleni mwanzoni mwa mwakani.

Mfugale, aliiomba serikali kukarabati barabara ya kijiji hicho kwani imekuwa kikwazo kupata huduma za jamii kutokana na ubovu.



## Mabilioni kuinua kipato cha wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Shilingi bilioni 100 zimetolewa kwa wakulima 50,000 nchini kwa ajili ya kuboresha kilimo na kuinua kipato.

Fedha hizo zimetolewa kwa wakulima hao wa Tanzania Bara na Zanzibar kutokana na ushirikiano wa Kampuni ya Yas na vyama vya ushirika 400 wakulima.

Ushirikiano huo pia umesaidia kuboresha maisha ya wakulima wadogo wa kahawa wa Wilaya za Karagwe na Kyerwa mkoani Kagera kupitia mbinu za ujumuishaji wa kifedha na kilimo endelevu.

Akizungumza kwenye hafla ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Chama cha Maendeleo ya Wakulima wa Kahawa Wilaya ya Karagwe (KADERE), Mwenyekiti wake, Leonard Kachebonaho, alisema hiyo ni fursa kwa wakulima katika wilaya hiyo kukuza uchumi wao.



Alisema wakulima watapata fursa mbalimbali kupitia ushirikiano huo kukuza kilimo chao cha kahawa na uchumi wao.

Ofisa Mkuu wa Mixx by Yas, Angelica Pesha, alisema wanatambua umuhimu wa teknolojia na huduma za kifedha kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii.

Alisema ushirikiano huo utaleta mabadiliko chanya kwa maisha ya wakulima wa Kagera na Kyerwa.

**Akizungumza kwenye hafla ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Chama cha Maendeleo ya Wakulima wa Kahawa Wilaya ya Karagwe (KADERE), Mwenyekiti wake, Leonard Kachebonaho, alisema hiyo ni fursa kwa wakulima katika wilaya hiyo kukuza uchumi wao.**

# Shule 100 kuunganishwa mkonga wa mawasiliano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHULE 100 visiwani hapa zinatarajiwa kuwekewa mkonga wa taifa wa mawasiliano ili kuboresha miundombinu ya kufundishia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema hatua hiyo itapunguza changamoto ya uhaba wa walimu hasa wa masomo ya sayansi na wananfunzi kukosa teknolojia kwa kuwa kila mmoja atatakiwa kusoma kidijitali.

Lela aliyasema hayo wizarani kwake katika hafla ya utiaji saini hati za ushirikiano na Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) ya kuweka mkonga huo kwa shule hizo.

Alisema lengo la Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuleta mageuzi katika sekta ya elimu visiwani hapa.

"Nichukue fursa hii kumpongeza Rais Mwinyi na serikali yake kuruhusu fedha hizi. Benki ya Dunia wanatoa dola milioni 1.5 kwa mradi huu na Kampuni ya Dolfen Dola 500,000. Serikali imejidhatiti katika mradi huu zaidi ya dola milioni tatu," alisema Waziri huyo.

Aliwataka walimu katika vituo vya kisayansi, TEHAMA na shule kubadilika na kusimamia walimu kutumia miundombimu hiyo kufundishia wanafunzi na kuwa wabunifu.

Alisema ni matumaini yake kuwa ZICTIA itafanya kazi hiyo kulingana na mkataba na kuhakikisha shule hizo zimeunganishwa na mkonga huo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khamis Abdalla Said, alisema baadhi ya shule hizo zitaunganishwa na mkonga huo kwa masharti ya kuwa na 'O data'.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Hawwah Mbaye, aliipongeza wizara hiyo kwa hatua hiyo na kwamba wanafarajika TEHAMA inashika kasi kwa jamii ambalo ni lengo la serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa ZICTIA, Shukuru Awadhi Suleiman, aliipongeza wizara hiyo ya elimu kwa kuunganisha shule hizo na mkonga huo na wanafunzi kuanza kusoma kwa kutumia teknolojia hiyo.

Suleiman, aliahidi mradi huo utakamilika kwa muda uliopangwa wa kipindi cha wiki 24.



Baadhi ya viongozi wa mabaraza ya vijana wa Shehia na Wilaya za Unguja wakisikiliza maelezo kutoka kwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, Ali Haji Hassan (hayupo pichani) katika mafunzo ya Afya ya Uzazi na Udhalilishaji huko Kituo cha Mafunzo ya Vijana (YTC) Bweleo wilaya ya Magharibi 'B'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahimizwa kutunza mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA), Sheha Mjaja amewataka wananchi kulinda mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi visiwani hapa.

Mjaja aliyasema hayo visiwani hapa wakati akifungua Jukwaa la Mwaka la Mashirikiano katika kubadilisha mawazo kwenye haki kwa jamii ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mabadiliko ya tabianchi ni moja ya changamoto inayovikabili visiwa vya Unguja na Pemba na kusababisha athari nyingi za kiuchumi kwa wananchi.

Alisema kuwa miongoni mwa sehemu zilizoathirika ni kilimo na kupanda kwa kina cha maji na kusababisha mmomonyoko wa ardhi baharini.

"Natoa wito kwa jamii kuendelea kupanda miti katika maeneo mnayoishi na kuilinda miti iliyokuwepo ili athari hizi tunazozipata zipungue au kuondoka kabisa," alisema.

Mjaja, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inaendelea kuhakikisha mabadiliko ya tabianchi yanafanyiwa kazi ili kuondoa athari kwa taifa.

Alisema sekta ya utalii visiwani hapa inahitaji kulindwa kwa kuwepo mazingira bora maeneo yote ya visiwa hivyo.

Mkurugenzi huyo, alipongeza Jumuiya ya Mwavuli wa Asasi za Kiraia visiwa vya Unguja na PEMBA 'ANGOZA' kwa kuiunga mkono Serikali kuhamasisha jamii umuhimu wa kutunza mazingira.

Mkuruenzi Mtendaji wa ANGOZA, Hassan Khamis Juma, alisema mabadiliko ya tabianchi yanaathiri makundi ya vijana, wazee na haki za binadamu ulimwenguni.

Wadau wa jukwaa hilo, walishauri njia mbadala kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo ongezeko la upandaji miti, bajeti na ushiriki wa Zanzibar kwenye mikutano ya kimataifa.



Baadhi ya viongozi mkoani Mara wakifuatilia mafunzo ya uraia na utawala bora yaliyofanyika mjini Musoma juzi, yakiratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bwana harusi aliyedaiwa kupotea akutwa kwa mganga wa kienyeji

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema bwana harusi, Vicent Masawe, mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, aliyetolewa taarifa ya kupotea baada ya harusi yake, amepatikana kwa mganga wa kienyeji kisiwani Pemba.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa Desemba 15, mwaka huu, Jeshi la Polisi lilimpata na kumshikilia Massawe, maarufu kama baba harusi kwa tuhuma za kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu (CDS/IR/2065/2024) na kutuhumiwa wizi wa kuminiwa (CDS/IR/2066/2024).

Kamanda Muliro alisema baada ya kutengeneza mazingira ya uongo ya kupotea na kutengeneza hisia kwa umma kuwa ametekwa, alikwenda kujificha Pemba, Chakechake Mgogoni kwa mganga wa kienyeji, Hamis khalid.

"Katika mahojiano ya kina kati ya polisi na mtuhumiwa baada ya kupatikana, alikiri kutenda makosa hayo na kwamba alilichua fedha kwa udanganyifu kutoka kwa watu mbalimbali ikiwa ni pamoja Sh. milioni 55 na gari aina Toyota Ractis lenye namba za usajili T620 EGU kwa udanganyifu kutoka kwa Sylvester Massawe.

"Alichukua tena Sh. milioni 10 kwa udanganyifu kutoka kwa Ramadhani, mkazi wa Magomeni. Alichukua fedha pia kwa udanganyifu Sh. milioni 15 kutoka kwa Ramadhani Bakari, mkazi wa Temeke.

"Mtuhumiwa alichukua fedha kwa udanganyifu Sh. milioni tano kutoka kwa Resma Mbuguni HR CBE (Ofisa Rasilimali Watu Chuo cha Elimu ya Boiashara). Pia alichukua Sh. milioni nne kutoka kwa Asia Mohamed, mkazi Madale kwa udanganyifu na alichukua tena Sh. milioni 1.5 kutoka kwa Ngoma, mkazi wa Kibaha," alisema.

Kamanda Muliro alisema mtuhumiwa aliendelea tena kwa udanganyifu na kuchukua Sh. milioni nane kutoka kwa Fauz Mussa, mkazi wa Tabata, baada ya kumwuzia gari ambalo si lake aliloliazima siku ya harusi yake namba T642 EGU Ractis mali ya Sylvester Massawe

SACP Muliro alisema Novemba 19, mwaka huu, polisi Kigamboni ilipokea taarifa ya kupotea kwa mfanyabiashara huyo ambaye ilidaiwa hakuonekana toka jana yake (Novemba 18) baada ya harusi yake.

Alisema alipotea huku akitumia gari Toyota Ractis ambalo baadaye lilibainika kuwa mtuhumiwa aliliuza badala ya kuirudisha kwa mwenyewe baada ya harusi yake Novemba 16, mwaka huu, kwenye ukumbi wa Golden Jubilee.

"Uchunguzi wa mashauri haya unaendelea na mtuhumiwa atafikishwa katika mamlaka nyingine za kisheria kwa hatua zaidi," ilisema taarifa hiyo.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi limetoa wito kwa wananchi kuwa watulivu pindi wapatapo taarifa kuhusiana na matukio ya namna hiyo, kwa kuviachia vyombo vya kiuchunguzi kufanyia kazi kwa kushirikiana na mamlaka zingine na wananchi.

"Jeshi la Polisi linawaonya na kuwatahadharisha kikundi cha watu wanne ambao kazi yao ni kujenga taharuki kwa umma.

"Kikundi hiki kila anayepotea au kutoonekana wao hujitokeza na kuandika kwenye mitandao ya kijamii kuwa watu hao wamechukuliwa na gari hard top nyeupe na kulazimisha hisia kuwa ni vyombo vya dola vimehusika.

"Malengo makubwa ya kundi hilo ni kutoa taarifa za uzushi zenye taharuki kwa lengo la kuichonganisha serikali, polisi na wananchi. Jeshi halitasita kuwachukulia hatua kali na za kisheria wahusika ili kukomesha tabia hizo," alionya.

Kamanda Muliro alisema wanaendelea kuwashukuru wananchi ambao wamekuwa wakitoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za kweli ambazo zinasaidia kufanikisha masuala ya kiuchunguzi.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

NDUGU **ABUDUNI ABUSWAI HASSANI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **TUKTUK WHITE 125** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.257 ARE.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ANAOMBWA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **MAS/B.1/6/VOL.XIII/524**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

NDUGU **ALLY SIRO ITAGOLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC475CCM.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/GEI/CHA/9262/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OLIVER MICHAEL AMANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC133DHJ** aina ya **BAJAJ BOXER.** Chassis No. **MD2A21BX8NWM92029,** Engine **No. PFXWNM22976.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/57401/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**NDG.SENDAMA PETER SENDAMA,** Anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo : 1) Cheti cha Chuo cha Uhasibu,Arusha,chenye Index na.**MPSM-01-0064-2022** cha mwaka 2023. 2) Academic Transcript,chenye Index na. **MPS-01-0064-2022,** KWA YEYOTE ATAKAYEVIONA ANAOMBWA KURIPOTI KWENYE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA ZA POLISI: **PHQ/RUV/SON/4817/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**YVONE JOHN PUNDA,** Anatangaza kupotea na cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **S4094/0051** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari ya wasichana St Martin Mwaka 2019. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/53774/2024**

# Mmarekani kizimbani tuhuma ulaghai dhahabu bandia

**NAIROBI, Kenya**

MAOFISA wanaochunguza ulaghai mkubwa wa dhahabu nchini Kenya wamemfikisha raia wa Marekani katika Mahakama ya Milimani kwa madai ya kushiriki katika ulaghai wa madini bandia yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 1.35 (Ksh. bilioni 3.1).

Ilielezwa kuwa mshukiwa huyo Antonucci Patrick alikamatwa alipowasili nchini Kenya akitokea Dubai, na kwamba alishtakiwa kwa kula njama ya kutenda uhalifu na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

Kwa mujibu wa Kurugenzi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), mtuhumiwa huyo anadaiwa alipanga ulaghai huo kwa kujifanya kama mfanyabiashara wa zamani wa benki, mwekezaji, na mshauri wa kisheria ambaye alibobea katika kuvinjari masoko yenye uhasama na tata, ambayo alidai yaliepukwa mara kwa mara na biashara za Marekani.

Pia ilielezwa kuwa kutokana na uchunguzi, Patrick alikutana na mlalamishi, raia mwenzake wa Marekani, Julai 2023 huko Las Vegas, Nevada. Akiwa amevutiwa na sifa zake, na kwamba mlalamikaji alimpa kandarasi ya kusimamia na kupata shughuli za dhahabu barani Afrika.

Mwathiriwa aliamini kuwa Patrick alipewa leseni na alilipa bonasi ya kutia saini ya dola 50,000 (Sh. milioni 116) Agosti 29, 2023, na kufuatiwa na malipo ya dola 15,000 (Sh. milioni 34) Januari 24, mwaka huu, na dola nyingine 15,000 Februari 28.

Ilielezwa kuwa wakati wa safari ya Nairobi, Patrick alimtambulisha mwathiriwa kama Caden Gebhard, Mmarekani mwingine ambaye alikuwa akijifanya kama mwanajeshi wa Marekani anayefanya kazi katika Kikosi Maalum cha 19. Gebhard alidaiwa kuonyeshwa kama mtu muhimu aliye na ushawishi mkubwa wa kikanda.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mlalamikaji alitambulishwa kwa mshirika wake kutoka Congo, Eric Mukendi, pamoja na anayedaiwa kuwa muuzaji dhahabu na msafirishaji nje ya nchi katika Hoteli ya Four Points huko Hurlingham, Nairobi.

Katika hatua hiyo, ilielezwa kuwa mwathirika kupitia kampuni yake ya AURUMSIC ONE LLC, alisaini Mkataba wa Mauzo na Ununuzi na Kampuni ya AERO Logistics kwa ununuzi wa kilo 2,820 za dhahabu.

Vile vile ilielezwa kuwa kati ya Machi 31, na Mei 30, mwaka huu, mwathirika alidaiwa kulipa dola 1,271,200 (Sh. bilioni 2.9) ili kufanikisha shughuli hiyo na kwamba hakuna shehena ya dhahabu iliyowahi kufikishwa, jambo lililomfanya mwathiriwa kuripoti suala hilo kwa mamlaka.

Ilielezwa kuwa Patrick alifikishwa mahakamani juzi, ambako alikana mashtaka hayo.

Huku Mahakama ya Milimani ikimpatia bondi ya Ksh milioni 10, ikiwa na hitaji la mdhamini mmoja wa Kenya.

Kesi hiyo imepangwa kutajwa tena Januari 23, 2025 kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Wakati huo huo, mamlaka ilithibitisha kuwa washirika zaidi wanaohusishwa na kashfa hiyo wanafuatiliwa huku uchunguzi ukiendelea.

DCI imetoa wito kwa jamii, haswa wanaohusika katika shughuli za thamani ya juu, kuwa waangalifu na kufanya uangalizi wa kina ili kuepuka kuathiriwa na njama hizo za ulaghai.

***Citizen Kenya***



Rais Mteule wa Marekani Donald Trump (wa kwanza kushoto) alipokutana na Rais Zelensky wa Ukraine na Emmanuel Macron wa Ufaransa (katikati). **PICHA: MTANDAO.**

# Trump aahidi kumaliza mauaji vita vya Ukraine

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS mteule wa Marekani Donald Trump amesema atafanya mazungumzo na viongozi wa Ukraine na Russia kumaliza alichokitaja kuwa 'umwagaji damu usiomithilika' kutokana na vita vya karibu miaka mitatu baina ya nchi hizo mbili.

Akizungumza kwa mara ya kwanza na waandishi wa habari tangu alipochaguliwa kuwa rais wa Marekani, Trump alisema ni lazima mauaji yanayotokana na vita hivyo yakomeshwe, akiahidi kwa mara nyingine kuumaliza mzozo huo atakapoingia madarakani. Alisema wanafanya mazungumzo na Rais wa Russia Vladimir Putin, pamoja na wawakilishi wa Zelensky na wa Ukraine, akisisitiza kwamba "Ni lazima tukomeshe vita na mauaji yasiyoelezeka."

Ilielezwa kuwa Trump mara kadhaa amedai kuwa na uwezo wa kumaliza mzozo wa Ukraine haraka lakini hadi sasa hajaweka wazi hadharani mkakati wake wa kufanya hivyo. Na kwamba hivi karibuni alitoa mwito wa kusitishwa mara moja kwa mapigano akisema „mazungumzo yanapaswa kuanza haraka."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Trump alikutana na Zelensky katika mkutano ulioandaliwa na Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa mwezi huu, baada ya kiongozi huyo wa Ukraine kusema kwamba serikali yake inatafuta amani ya kudumu na uhakika wa usalama.

Poland ambayo ni nchi mshirika muhimu wa Ukraine, imesema utawala wa Kyiv haupaswi kulazimishwa kufanya mazungumzo ya amani. Huku Waziri wa Mambo ya Nje wa taifa hilo Radoslaw Sikorski, akijenga hoja kwamba upande ulioanzisha uchokozi ndiyo unapaswa kulazimishwa kufanya mazungumzo.

Katika suala jingine, Trump aliashiria kwamba anaweza kutengua uamuzi wa hivi karibuni wa Rais Joe Biden wa kuruhusu vikosi vya Ukraine kutumia silaha za masafa marefu za Marekani kulenga maeneo ya ndani zaidi ya Russia.

***DW***

## Mahakama Uganda yaamuru serikali kuwalipa fidia waathiriwa wa uasi

**KAMPALA, Uganda**

MAHAKAMA ya Uganda imeamuru serikali kulipa fidia ya dola 2,740 (Sh. milioni 6.3) kwa kila mwathiriwa uasi wa kamanda wa kundi la waasi la 'Lord's Resistance Army' (LRA) Thomas Kwoyelo, aliyekuwa mwanachama wa kwanza mkuu wa kundi hilo kuhukumiwa na mahakama hiyo.

Wakati amri hiyo ya mahakama ikitolewa jana, ilielezwa kuwa Oktoba mwaka huu, Kwoyelo, alihukumiwa kifungo cha miaka 40 jela kwa uhalifu wa kivita ikiwa ni pamoja na mauaji, ubakaji, utumwa, utesaji na utekaji nyara.

Kulingana na uamuzi wa mahakama, ilielezwa kuwa ilibainika kwamba Kwoyelo alibainika kuwa hawezi kulipa fidia yoyote kwa waathiriwa kutokana na hali yake ya kiuchumi, na hivyo kusababisha mahakama kuamuru serikali kubeba gharama hiyo.

"Kiwango cha ukatili wa Kwoyelo, kulingana na uamuzi huo, ulikuwa wa dhihirisho la kushindwa kwa upande wa serikali ambayo inasababisha jukumu la mamlaka kulipa fidia kwa waathiriwa," uamuzi huo ulisema.

Ilielezwa kuwa Mahakama pia ilitoa fidia ya ziada ya pesa taslimu ya viwango tofauti kwa waathiriwa wa madhara mengine yaliyosababishwa na Kwoyelo, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mali na wizi.

Ilielezwa kuwa LRA iliyoanzishwa mwishoni mwa miaka ya 1980 kwa lengo la kuipindua serikali, iliwatendea ukatili Waganda chini ya uongozi wa Joseph Kony kwa takriban miaka 20 ilipopambana na wanajeshi kutoka kambi za kaskazini mwa Uganda.

Ilibainishwa kuwa vitendo vya waasi hao ni pamoja na ubakaji, utekaji nyara, kuwakata miguu na mikono na midomo ya waathiriwa na kutumia zana chafu kuwapiga watu hadi kufa.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mwaka 2005, chini ya shinikizo la kijeshi, LRA ilikimbilia kwenye misitu isiyo na sheria ya Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Jamhuri ya Afrika ya Kati, ambako pia ilifanya vurugu dhidi ya raia.

Ilielezwa kuwa makundi madogo madogo ndani ya LRA pamoja na Kony mwenyewe wanaaminika kuwa bado wanaishi katika maeneo hayo, ingawa mashambulizi sasa hayafanyiki mara kwa mara.

Jeshi la Uganda lilimkamata Kwoyelo mwaka 2009 kaskazini mashariki mwa Congo na kesi yake ikaingia katika mfumo wa mahakama ya taifa hilo hadi kuhukumiwa kwake mwezi Agosti.

***TRT***

# Straika GenGold FC awaburuza mastaa

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya timu yake kuburuza mkia katika Ligi Kuu Tanzania Bara, straika wa KenGold, Joshua Ibrahim, amefikisha mabao manne, yakiwa ni mengi zaidi kuliko waliyofunga washambuliaji maarufu na wa kigeni wa Simba na Yanga.

Jumapili iliyopita, Joshua alifunga bao moja katika mchezo wa Ligi Kuu wakati timu yake ikicheza dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, licha ya timu yake kufungwa mabao 3-2.

Licha ya KenGold kushika nafasi ya 16, ambayo ni ya mwisho chini ya msimamo ikiwa na pointi sita kwa michezo 14 iliyocheza, idadi ya mabao aliyofunga mchezaji hiyo ni kubwa zaidi kuliko mastraika wa Simba na Yanga ambao wengine walisajiliwa kwa mbwembwe, wakiwa na majina makubwa.

Straika huyo amewapiga kumbo, Leonel Ateba, Mcameroon wa Simba mwenye mabao matatu mpaka sasa kwenye Ligi Kuu huku Mganda Steva Mukwala, amefunga magoli mawili mpaka sawa na Valentino Mashaka, aliyepachika wavuni mabao mawili.

Jean Baleke wa Yanga, raia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), amefunga bao moja wakati Prince Dube ambaye ni raia wa Zimbabwe mpaka sasa hajafunga bao lolote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Takwimu zinaonyesha Simba na Yanga kwa sasa zinabebwa zaidi na viungo washambuliaji katika ufungaji wa mabao kuliko mastraika.

Kwa upande wa Simba, mchezaji ambaye amefunga mabao mengi zaidi mpaka sasa ni Jean Charles Ahoua, ambaye ana mabao matano mpaka sasa, ambapo upande wa Yanga mchezaji mwenye mabao mengi katika kikosi hicho pia, Pacome Zouzoua, aliyepachika mabao matatu.

Straika wa Singida Black Stars, raia wa Kenya, Elvis Rupia ndiye kinara wa ufungaji mabao hadi kufikia leo, akiwa amepachika mabao saba, akifuatiwa na washambuliaji wawili wa Fountain Gate, Selemani Mwalimu na Edgar William, wenye mabao matano kila mmoja, aliyepachika mabao matano, huku Ahoua, na Peter Lwasa wa Kagera Sugar, pia wakiwa na idadi hiyo ya mabao.

# JKT TANZANIA YAFUNGUKA LIGI KUU ITAKUWA 'HATARI'

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wakiwa katika maandalizi ya kucheza mechi zao mbili za viporo dhidi ya Simba na Namungo, uongozi wa JKT Tanzania umesema mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara utakuwa 'hatari zaidi', imeelezwa.

Ratiba mpya inaonyesha JKT Tanzania itaifuata Namungo keshokutwa, kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani, Lindi na itacheza kiporo chake cha pili dhidi ya Simba itafanyika Desemba 24, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, alisema ligi hiyo imekuwa na ushindani na hakuna mechi rahisi tofauti na ilivyokuwa misimu ya nyuma.

Bwire alisema ushindani huo wa msimu huu unadhihirishwa na tofauti ndogo ya pointi iliyopo katika msimamo wa ligi hiyo.

Aliongeza wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanafanya vyema katika mechi zao mbili za 'viporo' na wamejipanga kuvuna pointi kwenye michezo hiyo.

"Tunakwenda kukamilisha mzunguko wa kwanza, sisi tunakwenda kukamilisha viporo, mechi zote hizo tutakuwa ugenini, mzunguko wa kwanza umekuwa na ushindani mkubwa sana. Hii inaonyesha kwanza kumekuwa na ushindani mkubwa sana.

Hii inaonyesha ligi yetu ina ushindani, timu yetu timu zinapamba. Wajanja tayari tunaongezaongeza ili kuimarisha kikosi. Hii inaonyesha huko tunakokwenda mambo yatakuwa magumu zaidi," alisema Bwire.

Katika msimamo wa ligi, JKT Tanzania iko kwenye nafasi ya nane ikiwa na pointi 18 baada ya kucheza michezo 13 huku vinara wakiwa ni Azam FC yenye pointi 30 sawa na Singida Black Stars, zote hizo zimeshuka dimbani michezo 14.

Simba wako katika nafasi ya tatu wakiwa na pointi 28 wamecheza mechi 11 na wanafuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 27.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa Simba kuikaribisha KenGold FC kutoka jijini Mbeya kwenye Uwanja wa KMC Complex.




Kiungo mshambuliaji wa Pamba Jiji FC, Samuel Antwi (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. KMC ilipata ushindi wa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba Queens, Yanga zajiimarisha

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inajiimarisha zaidi, Simba Queens iko katika hatua za mwisho za kumsajili kipa Mkenya, Mercelina Cedar kutoka Gets Program.

Hata hivyo, Cedar ameshindwa kuitumikia Gets Program kutokana na uongozi wa timu hiyo kushindwa kukamilisha vibali vya kufanyia kazi nchini.

Taarifa zaidi zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema aliyekuwa kipa wa Simba Queens, Zubeda Mgunda, ametua katika kikosi cha Yanga Princess ili kuiongezea nguvu timu hiyo inayopambana kuwania taji la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa mara ya kwanza.

Zubeda ametua Yanga Princess akitokea Get Programs, ambayo imeshindwa kulea wachezaji wake kutokana na changamoto za kiuchumi zinazoikabili timu hiyo.

"Ameshamalizana na uongozi wa Yanga Princess katika dirisha dogo, ujio wake unaifanya Yanga kuwa na magolikipa wanne, Zubeda amesema yuko tayari kwenda kupata changamoto mpya," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza pia Yanga Princess imefanikisha usajili wa beki wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Diana Mnali, ambaye alikuwa pia akiichezea Gets Program.

Wakati huo huo, aliyekuwa Kocha Mkuu wa JKT Queens, Ali Ali, amejiunga rasmi na kikosi cha Mashujaa Queens.

"Ni utaratibu wa ndani wa taasisi, Ali sasa ndiye ataiongoza Mashujaa Queens. Lakini pia kuna wachezaji wapya wataongezwa na wengine wataachwa baada ya ujio wa kocha huyo, kwa wale wasiomjua Ali, ndiye aliyewapa ubingwa mara tatu JKT Queens," kiliongeza chanzo chetu.

Simba Queens yenye pointi 16 ndio vinara wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMUUZA RASHFORD

MANCHESTER United imesema inamuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27, na itaidhinisha uhamisho wa bei ya chini ifikapo Januari. ***(Gurad)***

### SALAH, LIVERPOOL SAFI

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32, anakaribia kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya England. ***(Marca)***

### ROHL AKARIBIA SHEFFIELD

KLABU ya Southampton inafikiria kumnunua Kocha wa Sheffield Wednesday mwenye umri wa miaka 35 ambaye ni raia wa Ujerumani, Danny Rohl, baada ya kumfukuza Russell Martin. ***(Times)***

### WIRTZ HAKIJAELEWEKA

UHAMISHO wa majira ya kiangazi kuelekea Bayern Munich, Real Madrid au Manchester City kwa sasa haupo mezani kwa Mjerumani mwenye umri wa miaka 21 na kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen, Florian Wirtz, ambaye anatazamiwa kuongeza mkataba wake hadi kufikia mwaka 2028. ***(Sky Germany)***

### STERLING KUBAKIA ARSENAL

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling, mwenye umri wa miaka 30 hana mpango wa kukatiza uhamisho wake wa mkopo katika klabu ya Arsenal licha ya kutopata namba. ***(Standard)***

### KIWIOR NJIA MOJA

MLINZI wa Arsenal, Jakub Kiwior, mwenye umri wa miaka 24 ameamua kuondoka kwa washikabunduki hao Januari, huku Napoli ikimtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland. ***(Il Mattino)***

### KOSTOULAS KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inamsaka mshambuliaji wa Olympiacos ya Ugiriki, Charalampos, Kostoulas, mwenye umri wa miaka 17. ***(Sun)***

### PALMEIRAS: REIS HAUZWI

OFA ya Brighton ya pauni milioni 20.7 kwa ajili ya Mbrazil, Vitor Reis (18), imekataliwa, huku Palmeiras ikiwa tayari kujadili mustakabali wa beki huyo baada ya mashindano ya Kombe la Klabu bingwa ya Dunia kumalizika. ***(ESPN Brazil)***

### AGOUME ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inamfuatilia kwa karibu kiungo wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Lucien Agoume, mwenye umri wa miaka 22 kama mbadala wa kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey (31). ***(FootballTransfers)***

### BENZEMA AFIKIRIA KUSTAAFU

MSHAMBULIAJI wa Al-Ittihad na Ufaransa, Karim Benzema, mwenye umri wa miaka 36 anafikiria kustaafu mapema mwishoni mwa msimu wa 2024-25. ***(Relevo)***

### DELE ALLI KITAELEWEKA

KIUNGO wa kati wa zamani wa Hispania, Cesc Fabregas, ambaye sasa ni Kocha wa Como, amempa, Dele Alli, mwenye umri wa miaka 28, fursa ya kufanya mazoezi na timu yake kuanzia Januari. ***(ESPN)***

## DONDO SOKA MAGAZ ULAYA



# LOOKMAN MWANASOKA BORA WA AFRIKA 2024

## ●●●Mshindi huyo raia wa Nigeria asema tuzo hiyo ya CAF ni baraka na...

**MARRAKECH, Morocco**

ADEMOLA Lookman alitwaa tuzo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ya Mwanasoka Bora wa mwaka wa Afrika katika hafla iliyofanyika jijini Marrakech nchini, Morocco juzi usiku baada ya msimu mzuri akiwa na Klabu ya Atalanta na Timu ya Taifa ya Nigeria.

Mchezaji wa Zambia, Barbara Banda alishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa kike wa baada ya kuipa ubingwa wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake ya Marekani, Orlando Pride na alifunga bao la ushindi katika fainali dhidi ya Washington Spirit.

Golikipa wa Afrika Kusini na Klabu ya Mamelodi Sundowns, Ronwen Williams, alitwaa tuzo ya golikipa bora wa mwaka na mchezaji bora wa ndani.

Lookman mwenye umri wa miaka 27, alifunga hat-trick katika fainali ya Ligi ya Europa na kuipatia Atalanta inayoshiriki Serie A taji lao la kwanza la Ulaya, na taji la pili kuu katika historia ya klabu hiyo ya yenye miaka 117.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa RB Leipzig, Leicester na Fulham pia alifunga mara tatu Nigeria ilipotinga fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2024, ambapo walifungwa na Ivory Coast kwa bao la lala salama la Sebastian Haller.

Lookman alifunga mabao 17 na kutoa asisti 10 katika michezo 45 katika mashindano yote kwa Atalanta msimu wa 2023-24 na ameanza vyema kampeni hii, akifunga magoli 11 katika michezo 19.

"Tuzo hii ni baraka, kutambuliwa kama mchezaji bora wa Afrika ni jambo la kushangaza," alisema Lookman mara baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo.

"Miaka minne iliyopita kazi yangu ilishuka, lakini sasa niko hapa kama mchezaji bora zaidi barani Afrika. Usiruhusu kushindwa na kuzuia ndoto zako."

Lookman katika tuzo hiyo aliwashinda Achraf Hakimi wa Morocco, mlinda mlango wa Afrika Kusini, Ronwen Williams, fowadi wa Borussia Dortmund, Serhou Guirassy na winga wa Brighton na raia wa Ivory Coast, Simon Adingra.

Nigeria imetwaa tuzo hiyo kwa mara ya pili mfululizo, baada ya mwaka jana kuchukuliwa na mchezaji mwenzake na Lookman, Victor Osimhen. Tuzo hiyo ilianza kutolewa kwa mara ya kwanza na CAF mwaka 1992.

Sadio Mané, Mohamed Salah, Pierre- Emerick Aubameyang na Riyad Mahrez wote wameshinda tuzo hiyo katika miaka ya hivi karibuni.

Samuel Eto'o na Yaya Toure ndio wanaoshikilia rekodi ya kushinda mara nyingi zaidi, kila mmoja akitwaa tuzo hiyo mara nne. Tuzo nyingine zilichukuliwa na:

**Kocha Bora wa Wanaume:** Emerse Fae (Ivory Coast)
**Kocha Bora wa Wanawake:** Lamia Boumehdi (TP Mazembe)
**Golikipa Bora Wanawake:** Chiamaka Nnadozie (Nigeria & Paris FC)
**Klabu Bora Wanaume:** Al Ahly (Misri)
**Klabu Bora Wanawake:** TP Mazembe (Jamhuri ya Congo)
**Mchezaji Chipukizi Wanaume:** Lamine Camara (Senegal & Monaco)
**Mchezaji chipukuzi Wanawake:** Doha El Madani (Morocco & AS Far)
**Timu Bora Wanaume:** Ivory Coast
**Timu Bora Wanawake:** Nigeria

HABARI MICHEZO

# Yamal kusaini mkataba Barca

**BARCELONA, Hispania**

WAKALA, Jorge Mendes, amefichua bila shaka yoyote, Lamine Yamal, atasaini mkataba mpya na Barcelona.



Yamal ambaye anaonekana kuwa mrithi wa kiti cha enzi cha Lionel Messi – kwa mujibu wa wakala huyo, alisema nyota huyo msimu amechangia moja kwa moja kufunga mabao 17 katika mechi 21 kwenye mashindano yote.

Katika msimu wa joto, wakati Yamal alipokuwa akisherehekea siku yake ya kuzaliwa ya kutimiza umri wa miaka 17 na kushinda Euro 2024, alitajwa anawaniwa na Paris Saint-Germain. Kama ilivyothibitishwa baadaye, Barcelona ilipokea ofa iliyovunja rekodi ya dunia ya euro milioni 250 kutoka kwa mabingwa hao wa Ufaransa wakati wa michuano hiyo.

Lakini Barcelona walikataa kwa uwazi ombi hilo ambalo halikuwa jaribio la kwanza la PSG kutaka kumtoa Yamal pale Katalunya.

Mkataba wa sasa wa Yamal utaendelea hadi msimu wa joto wa 2026, lakini anajivunia kifungu cha kuachiwa cha euro Bilioni moja - kiasi ambacho hata PSG watapata shida kukifikia.

Alipoulizwa swali kuhusu suala hilo wiki hii, wakala wa Yamal, Mendes alisema: „Bila shaka Lamine Yamal atasaini mkataba mpya Barcelona.“

Makadirio ya sasa yanaonyesha Yamal anapata mshahara wa euri 32,000 kwa wiki.

Kiasi hicho kinalinganishwa na wahitimu wengine wa akademi ya Barcelona ambao bado hawajasaini mkataba mpya, lakini ni ndogo ukilinganisha na wachezaji wengine waandamizi wa kikosi hicho. Hata Pau Cubarsi, ambaye bado ‚analala‘ katika klabu ya La Masia, anapata zaidi ya mara mbili ya Yamal.

# VAN DIJK AIONYA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amewaonya wachezaji wenzake wa Liverpool, majeraha na adhabu kwa wachezaji yanaweza kuamua hatima ya mbio zao za ubingwa wa Ligi Kuu England.



Wekundu hao wapo kileleni mwa msimamo, pointi mbili mbele ya Chelsea wakiwa wamecheza mechi moja pungufu, lakini sasa wanapaswa kujiandaa kucheza bila beki wa kushoto, Andy Robertson, ambaye alitolewa kwa kadi nyekundu mapema katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Fulham.

Matokeo hayo yanawaacha Liverpool kuwa na upungufu kwenye ulinzi, ambapo Ibrahima Konate na Conor Bradley wote ni majeruhi na Kostas Tsimikas anarejea tu kutoka tatizo lake la utimamu wa mwili, na Van Dijk alikiri vipindi kama hivi vinaweza kusaidia sana katika kuamua ni timu gani itashinda taji la Ligi Kuu England.

“Wacha tuone kitakachotokea,“ alisema Van Dijk kabla ya mechi ya robo fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Southampton itakayochezwa leo.

„Sijui, labda kocha lazima awe mbunifu.

„Majeraha yaliyopo tunapaswa kuyakubali na kuyashughulikia, kwa bahati mbaya bila shaka, lakini tunatumaini mambo yatabadilika na wachezaji watarejea haraka iwezekanavyo kwa njia bora zaidi.

“Imetajwa mara nyingi, majeruhi yanaongezeka, unaona hivyo kwa timu tofauti, na kiasi cha michezo tunayocheza. Kisha majeraha yatatokea na hiyo inaweza kubadilisha ubora wa michezo pia.

“Lakini nini Manchester City wamekuwa wakipitia majeraha na michezo isiyo na msimamo kwa kupanda na kushuka.

“Sitazungumza juu yao kwa sababu siwaangazii lakini najua jinsi ilivyo ngumu kupitia hilo na natumaini hatutapitia hilo.”



# MAGUIRE: NITABAKIA MANCHESTER UNITED

**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire amesema hajakata tamaa ya kuongeza muda wake wa kukaa Manchester United baada ya kufanya mazungumzo ‘chanya’ kuhusu mkataba mpya.

Mkataba wa sasa wa Maguire unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa United wana chaguo la kumwongezea mwaka mmoja hadi kufikia mwaka 2026.

Beki huyo wa England alikaribia kuondoka Old Trafford kwenda West Ham mwaka jana kabla ya uhamisho kushindikana.

Amekuwa hana namba ya kudumu na kushuka kiwango baada ya kuwasili kwa Matthijs de Ligt na Leny Yoro majira ya joto.

Lakini baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika ushindi wa mabao 2-1 wakati United ilipowachapa Manchester City Jumapili iliyopita, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 bado ana matumaini ya kubaki.

“Sijafikiria sana kuhusu hatima yangu,“ alisema Maguire.

“Bado nina mwaka huu kwenda na chaguo mikononi mwao. Lakini dalili zote ni chanya kwa sasa.“

Alipoulizwa kama mazungumzo kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu yanaendelea, Maguire alijibu: „Ndio.“

Maguire alijumuishwa katika kikosi cha Ruben Amorim kwenye Uwanja wa Etihad. Lakini mchezaji huyo wa zamani wa Leicester City alimfanya Erling Haaland kuwa kimya kabla ya United kufunga mabao mawili ya dakika za lala salama na kupata ushindi mnono kwenye dabi hiyo.

“Umekuwa mwanzo mgumu wa msimu kwetu na sio sana kwa mashabiki wetu kushangilia, kwa hiyo ni kwa ajili yao,“ aliongeza Maguire.

“Nilidhani mchezo ulikuwa wa 50-50, kusema ukweli. Ningeweza kwenda kwa njia yoyote ile. Ni uboreshaji lakini bado ni safari ndefu.“

HABARI MICHEZO

# KALLY: SIJAFURAHISHWA NA KIWANGO CHA KMC BARA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata ushindi, Kocha Mkuu wa KMC, Kally Ongalla, amesema bado hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kally, alisema kitu pekee alichofurahia katika mchezo huo ni kupata pointi tatu ambazo zimewasogeza juu ya msimamo lakini si vinginevyo.

Kally alisema wachezaji wake walicheza kiwango cha chini na kuwapa nafasi wapinzani wao kumiliki mpira bila kuwapa presha.

Kocha huyo alisema wanarejea tena kwenye uwanja wa mazoezi ili kurekebisha hali hiyo.

"Bado safari ni ndefu, sijaridhishwa na kiwango cha wachezaji wangu, kwa pointi tatu sawa, lakini kwenye uchezaji bado, tumewapa nafasi sana wapinzani wetu kumiliki mpira bila kuwapa presha yoyote.

Baada ya kuona mambo hayaendi nilibadilisha ‚plan' na nikaamua kuchezesha mastraika wawili, hii imetusaidia sana kupata ushindi, vinginevyo hali ingekuwa tofauti," alisema kocha huyo.

Ushindi huo umeifanya KMC kupaa hadi nafasi ya tisa ya msimamo ikifikisha pointi 18, ikiwa imeshamaliza michezo yake ya 15 ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Naye Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Fred Minziro, alisema kipindi cha kwanza wangeweza kuimaliza mechi kama wangetumia vizuri nafasi walizotengeneza na kuongeza walimiliki mpira wa kiasi kikubwa.

Minziro alisema alifurahia viwango vya wachezaji wake wapya, Deus Kaseke na Habib Kyombo, ambao walicheza kwa mara ya kwanza katika kikosi hicho, wakisajiliwa kipindi cha dirisha dogo mara tu baada ya kufunguliwa.

"Kipindi cha kwanza tungeweza 'kuia' mechi kama tungekuwa makini, wachezaji walioongezeka wameleta chachu kwenye mchezo huu licha ya kupoteza, nadhani watakuwa msaada mkubwa kwenye timu," alisema Minziro.

Bao pekee katika mchezo huo liliifungwa na Hans Masoud.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), dhidi ya Kenya itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini Kampala, Uganda. **PICHA: TFF**

# Serengeti Boys karata muhimu

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), inakutana na yosso wenzao wa Kenya katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini, Kampala nchini Uganda.

Katika mechi ya kwanza ya Kundi A, Serengeti Boys ilitoka sare ya bao 1-1 na wenyeji Uganda na leo inahitaji ushindi wowote ili kufuzu hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Aggrey Moris, alisema wachezaji wake wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo ambao ni muhimu ili kusonga mbele. Moris alisema watashuka uwanjani kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu Kenya pia itahitaji kupata matokeo chanya ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kucheza hatua inayofuata.

"Tunaenda kucheza mechi muhimu, tunajua Kenya pia inawachezaji wenye uwezo, tumewaandaa vijana kuongeza umakini na utulivu wanapokaribia katika lango la mpinzani, tumejipanga kupambana ili kupata ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa leo ni kati ya Sudan Kusini dhidi ya Sudan.

Sudan Kusini watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0 waliopata katika mechi ya kwanza ya Kundi B dhidi ya Somalia.

Fainali ya mashindano hayo yanayoshirikisha timu sita kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itachezwa Desemba 27, mwaka huu.

## Mrithi wa Diarra

INATOKA UK. 24

kuaminika.

"Amecheza vizuri kwa kujiamini, sasa hata akiumia Diarra wanachama na mashabiki wa Yanga hawatakuwa tena na wasiwasi wa mtu atakayeshika nafasi yake, tumpongeze na tunaamini atakuwa na mwendelezo huo siku zote," aliongeza ofisa huyo.

Katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Khomeini amedaka michezo miwili na yote alidaka dakika 90 bila kuruhusu bao.

Alidaka katika mchezo wa Yanga dhidi ya Coastal Union uliochezwa Oktoba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha ambapo mabinga hao watetezi walishinda bao 1-0 na Novemba 30, mwaka huu timu yake ilipokuwa ugenini dhidi ya Namungo na kushinda mabao 2-0.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kimeingia kambini mara baada ya kurejea nchini kutoka DR Congo, kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Mashujaa FC kutoka Kigoma itakayochezwa kesho

Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema atabadilisha mfumo aliocheza dhidi ya TP Mazembe, kutokana na kuona timu za Ligi Kuu Tanzania Bara zikikabia zaidi chini.

Katika msimamo wa Yanga yenye pointi 27 iko kwenye nafasi ya nne nyuma ya vinara Singida Black Stars, Azam FC zenye pointi 30 kila moja na Simba yenye pointi 28.

## Simba yaitisha KenGold FC

INATOKA UK. 24

zinapocheza nao hata kama ipo chini katika msimamo wa ligi hiyo.

„Kila mechi ambayo Simba inacheza ni fainali, haijalishi KenGold ipo nafasi ya ngapi, hatujawahi kudharau mechi yoyote, na hii timu wala siyo timu mbovu kama inavyosemwa, ni matokeo tu, sisi wachezaji tumejiandaa vizuri sana tuna imani mchezo utakuwa bora na tutashinda," alisema Awesu aliyesajiliwa msimu huu akitokea KMC.

Naye Kocha Mkuu wa KenGold, Omari Kapilima, alisema timu yake imejiandaa vyema kukabiliana na Simba katika mchezo huo wanaotarajia utakuwa mgumu.

"Tumejiandaa vizuri, Simba ni timu kubwa, ina benchi bora la ufundi na wachezaji wa kiwango cha hali ya juu, lakini na sisi tumejiandaa kukabiliana nao," Kapilima alisema.

Aliongeza amewataka wachezaji wake kuongeza utulivu katika mchezo huo na anaamini wakiwa makini wanaweza kuondoka na pointi tatu.

Kwa sasa Simba iko katika nafasi ya tatu ya kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 28 baada ya kucheza michezo 11 wakati KenGold iliyoshuka dimbani michezo 14 inaburuza mkia ikiwa na pointi sita kibindoni.

KenGold imeshinda mchezo mmoja, sare tatu na imepoteza michezo 10.

Michezo
Jumatano Desemba 18, 2024
Nipashe

Lookman Mwanasoka Bora wa Afrika 2024

UKURASA 21



# MRITHI WA DIARRA ATAFUTWA YANGA

Khomeini atajwa kubeba mikoba endapo ataendelea kuonyesha...

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga umesema endapo kipa, Khomeini Aboubakar, atakuwa na mwendelezo mzuri, wanaamini anafaa kuwa mrithi sahihi wa kipa wao namba moja wa sasa, Djigui Diarra, ambaye ni raia wa Mali, imeelezwa.

Khomeini aliingia katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe iliyochezwa ugenini Mjini Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo) baada ya Diarra kuumia.

Kabla ya kuumia huko DR Congo, Diarra aliruhusu kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC na baadaye nyavu zake zikatikiswa tena Yanga ilipofungwa magoli 3-1 na Tabora United, mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Diarra pia aliruhusu nyavu zake kutikiswa mara mbili walipocheza mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal ya Sudan na alifungwa idadi kama hiyo ya mabao walipokutana ugenini na MC Alger kwenye michuano hiyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema Khomein alionesha kiwango kizuri kwa dakika 45 za kipindi cha pili alizocheza katika mchezo huo uliochezwa Jumamosi iliyopita na kuongeza anaonekana atakuwa kuwa kipa wa kiwango cha juu nchini Tanzania.

Kamwe alisema baada ya kipa huyo kuchukua mikoba ya Diarra, viongozi walikuwa na wasiwasi na walipata mshangao kuona amefanya vyema muda wote alioku-wa langoni.

"Tunaamini kama atakuwa na mwendelezo ule tuliouona DR Congo, atakuja kuwa golikipa mzuri siyo kwa Yanga tu bali hata kwa taifa, unajua hakuna aliyeamini kama angeweza kudaka vile baada ya kuumia kwa Diarra, kila mmoja alikuwa na wasiwasi, lakini dakika 45 za pili alisimama imara langoni, hakuruhusu bao lolote," alisema Kamwe.

Katika mchezo huo, Diarra aliumia ingawa alijitahidi kuendelea na mchezo, lakini hakurejea tena uwanjani baada ya mapumziko na Khomeini, aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu akitokea Singida Black Stars akasimama langoni.

"Aliniambia ilikuwa ni mechi yake ya kwanza kimataifa na akasema ametimiza ndoto yake kwa sababu hakuamini kitu kama hicho kama anaweza kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tena timu ikiwa ugenini, kwa hiyo amefurahi sana na imemwongezea kujiamini," Kamwe alisema.

Aliongeza pamoja na huenda akawa mrithi sahihi wa Diarra, lakini kwa sasa wanachama na mashabiki wa Yanga hawatakuwa na wasiwasi kama kipa huyo akiwa nje, kwa sababu kiwango alichowaonyesha katika mechi hiyo ya kimataifa kimempa nafasi ya kuanza

INAENDELEA UK. 23

## SIMBA YAITISHA KENGOLD



Mpanzu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumaliza majukumu ya mashindano ya kimataifa, Simba inatarajia kukutana na KenGold ikitamba haitakuwa na huruma katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema watashuka kwa heshima na kamwe hawatawadharau KenGold kwa sababu inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Fadlu alisema wanakwenda kukabiliana na timu hiyo wakifahamu wametoka kupoteza mechi iliyopita waliyocheza na Namungo licha ya wao kuanza kuongeza kwa mabao 2-0.

"Tunakwenda kucheza dhidi ya KenGold, ni timu iliyotoka kupoteza kwa kufungwa mabao 3-2 dhidi ya Namungo, lakini ikiwa imetangulia kwa kufunga mabao 2-0, tumeichunguza na kujua inacheza vipi na taarifa nyingine ambazo zinabaki mikononi wetu, lakini kifupi wanazuia zaidi na kushambulia kwa kushtukiza wakiwa na mawinga wao katika mbio, tumeliona hilo, sisi tunasema hatutaidharau timu hiyo, ila hatutaionea huruma," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Mara ya mwisho Simba kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ilikuwa Novemba 22, mwaka huu ikiwafunga Pamba Jiji bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza, bao la penalti lililofungwa na Leonel Ateba.

Inakwenda kucheza mchezo huo, siku tatu tu baada ya kumaliza kucheza mechi ya raundi ya tatu ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, hatua ya makundi dhidi ya CS Sfaxien kutoka Tunisia, Mnyama akishinda mabao 2-1, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Awesu Awesu, aliliambia gazeti hili wachezaji wote wamejipanga kuhakikisha wanapata ushindi na hawaidharau hata chembe KenGold, kwa sababu timu zote za Ligi Kuu hupania zaidi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >